Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

"Hamtaweza kuufikia wema hasa mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda; na chochote mnachokitoa, basi hakika Allah Anakijua." (3:93)

JUZU 77 No. 191 | RABIUL AWWAL 1439 AH | NOVEMBA 2017 | NUBUWWAT 1396 HS | BEI TSH. 500/=

Khalifa Mtukufu apongeza moyo wa kujitolea wa Waahmadiyya

Atangaza mwaka wa 84 wa Tahrik Jadid.

Na Mwandishi Wetu

Hadhrat Khalifatul Masih V atba, (Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani) alitoa hotuba katika msikiti wa Baitul Futuh mjini London, ambapo alipongeza moyo wa kujitolea wa Waahmadiyya sambamba na kutangaza mwaka wa 84 wa Tahrik Jadid.

Baada ya *Tashahhud, Taa'udh* na *Surat Fatihah* Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisoma Aya ifuatayo:

"Hamtaweza kuufikia wema hasa mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda; na chochote mnachokitoa, basi hakika Allah Anakijua." (3:93)

Katika Aya hii Allah Mtukufu Anazungumzia somo ambalo siku zote linaeleweka vizuri na wale walioamini, na wale wanaojitolea katika njia ya Allah. Masahaba wa Mtukufu Mtume (saw) walijitolea maisha yao, mali na muda wao kwa ajili ya imani yao. Ni katika wale walioelewa kiini cha *al-birr* (Ucha Mungu). Kwa maneno mengine walielewa na walifanya juhudi kufikia viwango vya juu vya ucha Mungu, utawa, khulka, kujitolea, mali na kupata radhi ya Allah Mtukufu.



Sehemu ya waumini ndani ya Baitul Futuh, msikiti uliopo jijini London ambao Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. hutoa hotuba zake za Ijumaa na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Sambamba na hilo, imesimuliwa kuwa wakati aya iliyotajwa hapo awali ilipofunuliwa, Hazrat Abu Talha (ra) alimwambia Mtukufu Mtume (saw), "Ewe Mjumbe wa Allah! Ninamiliki bustani ya matunda, ambayo inajulikana kama Birr Rauhah. Miongoni mwa mali zangu, hii bustani ya matunda ni kitu ninachokipenda kuliko vingine.

Endelea uk. 3

Jalsa Salana 2017 yapata Mabadiliko makubwa

Na Mwandishi Wetu

Mnamo Mei 1888 katika kijiji kidogo na kisichojulikana (wakati huo India ikiwa koloni la Uingereza) kwa jina Qadian, chini ya ufunuo wa kiungu, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alitangaza ya kuwa yeye ni Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi aliyekuwa akisubiriwa na Waislamu wote. Baadaye mwaka huo huo alifanya Jalsa Salana ya kwanza ambayo ilihudhuriwa na washiriki 75. Akielezea lengo la Jalsa Salana, Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema "lengo kuu la mkusanyiko huu ni kuwa wanajumuiya wanyofu waweze kupata faida za kiroho na wakati huo huo waongeze elimu zaidi na kupiga hatua katika ufikiaji wa malengo yao. Kwa kufuatisha nyayo za Masihi Aliyeahidiwa a.s. Jalsa Salana zinafanywa katika nchi mbalimbali duniani ambako kuna waahmadiyya.....



Amir na Mbashiri Mkuu akitoa neno la utangulizi kwa Mh. Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliposhiriki Jalsa Salana ya 2017. Kushotoni mwa Waziri MKuu ni Naibu Amir Jamaat, Ndugu Issa Mwakitalima

(Jalsa Salana yaani mkutano wa mwaka hufanyika). Jalsa Salana hufanyika katika nchi mbalimbali kama Uingereza, Kanada, Marekani, India, Pakistan, na Afrika katika nchi kama Nigeria na Ghana wamekuwa wakifanya Jalsa Salana zenye mafanikio sana. Kabla ya 1961, Afrika ya Mashariki ilikuwa moja kijamaat. Ilikuwa ni uhuru wa Tanganyika 9 Disemba 1961 ambapo palitokea Uganda, Kenya na Tanganyika ambayo ni Tanzania ya leo chini ya Sheikh Muhammad Munawwar. Jalsa Salana nchini Tanzania imeanza kuhesabiwa rasmi 1968 ambayo ndiyo ya kwanza. Jalsa Salana zetu mbili zilipata baraka za uwepo wa Khalifatul Masih wa IV,

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Mkutano Mkuu wa 48 wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya mwaka huu, Jalsa Salana 2017, ulipata heshima ya kipekee ya kuhudhuriwa na Waziri Mkuu wa serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Majaliwa Kassimu Majaliwa. Ujio wa Kiongozi huyo wa ngazi za juu ya serikali haukuwa ukitarajiwa na wengi miongoni mwetu ukizingatia kuwa hapakuwahipo kuwa na taarifa rasmi za ujaji wake kabla na baada ya kuanza kwa mkutano huu ambao huwakutanisha wanajamaati kutoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani pamoja na wageni waalikwa kutoka nchi mbalimbali. Hivyo, ujio wake ulikuwa na msisimko mkubwa kwa wahudhuriaji na heshima ya kipekee ya serikali kwa Jumuiya yetu. Nasi hatuna budi kusema, Alhamdulillahi.

Ingawaje hii si mara ya kwanza kwa viongozi wa Serikali, hasa wenye hadhi ya Mheshimiwa Majaliwa kuhudhuria katika mikutano yetu,la, bali ni kawaida ya Mikutano ya Jamaat kualika watu mbalimbali kutoka serikalini ama taasisi mbalimbali na watu binafsi ili waweze kushiriki na kujionea Uislamu wa kweli nje ya propaganda za maadui wa Jamaat.

Kumbukumbu zinaonesha ya Kwamba viongozi wengi wa Serikali waliwahi kufika katika mikutano yetu wakiwemo Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Aliyekuwa Waziri Mkuu wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Frederick Sumaye, Mawaziri na viongozi wa ngazi mabalimbali za serikali pamoja na taasisi binafsi , kwa kutaja wachache. Bali, ujio wake mwaka huu umetukumbusha jambo moja la maana sana kuwa 'Jalsa Salana Ni Mkutano wenye Baraka Nyingi, Kuikosa ni Kukosa Mengi'.

Baraka za Jalsa Salana ni nyingi kiasi ambacho ukitaka kuzihesabu peke yako ni sawa kujipa mzigo mkubwa ambao kuubeba peke yako si jambo lenye kufaa sana maana kwa akali kila mmoja huyatazama mambo kwa namna ya uelewa wake, ila si vibaya kila mshiriki atazame yeye mwenyewe ni kwa nmna gani ameridhika na kila hatua ya ushiriki wake pamoja matokeo chanya yenye kuonekana na yale yaliyofichika katika upeo wake.

Naam, kwetu ujaji wa Waziri Mkuu ulikuwa ni heshima ya kipekee ambayo imetokana na kuimarika kwa mahusiano mema pamoja na historia iliyotukuka ya Jamaat katika harakati za kuikomboa nchi yetu kutoka katika mikono ya wakoloni wa Kiingereza mwanzoni mwa miaka ya 60. Ni uadilifu, uaminifu na kujitoa kwa hali ya juu kulikofanywa na baadhi ya wanajamaat waliopata nyadhifa mbalimbali za kuitumikia serikali pia ni jambo linalopigilia msumari katika mahusiano haya ambayo ni nadra kuyashuhudia kwa wenzetu.

Mtume SAW ametukumbusha kuwa 'Yule ambaye hamshukuru kiumbe mwenzake kwa wema aliofanyiwa, hawezi kumshukuru Allah Mwenye Enzi'.

Ni katika hali hiyo ya heshima na unyenyekevu nasi hatuna budi kushukuru kwa heshima tuliyopewa na serikali yetu ya awamu ya Tano chini Rais John Pombe Magufuli ambaye alitutumia salamu zake kupitia Waziri Mkuu. Allah Azidi Kuibariki Nchi Yetu na Kuilinda dhidi ya fitina na maadui ambao hawaoni tabu kuwaona wengine wakiwa na amani hii tuliyonayo.

Jalsa Salana 2017 yapata Mabadiliko makubwa

Kutoka uk. 1

Hadhrat MIrza Tahir Ahmad r.h mwaka 1988 na Khalifatul Masih V, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a mwaka 2005. Kwa miaka kadhaa hatukuwa na kumbi rasmi kwa Jalsa Salana zetu. Tulifanyia Jalsa katika madarasa na viwanja vya wazi. Kwa fadhila za Allah baada ya kupata eneo letu Kitonga, tunalo sasa eneo la kudumu na stahiki kwa ajili ya Jalsa Salana. Kitonga tuna Jalsa Gah kubwa iliyo katika sehemu mbili; moja kwa kina mama na nyingine kwa wanaume. Shughuli kadhaa zamekuwa zikifanyika katika kuisherehekea Jalsa Salana kama utoaji damu na mpira wa miguu.

Hiki ndicho kilichotukia wakati Jamaat Ahmadiyya Tanzania ilipofanya Jalsa Salana yake ya 48 mnamo 29, 30 Septemba hadi mosi Oktoba 2017. Bila ya shaka ilikuwa ni Jalsa yenye msisimko na ya kukumbukwa ambayo iliacha alama katika ukurasa wa historia yetu. Maandalizi kwa ajili ya dhifa hii ya kiroho yalianza siku za usoni mwa Julai na kuendelea hadi Septemba. Kamati za Jalsa zilikuwa zikichakalika na masuala mbalimbali ya Ualikaji wageni, Habari na MTA, Chakula, Malezi, Malazi, Ulinzi, Maonyesho, Usafirishaji, Mapambo na Usajili. Kamati zote zilifanya kazi usiku na mchana kuhakikisha "kila jiwe limepinduliwa"

Jalsa ilifunguliwa kwa upandishaji wa bendera ya Ahmadiyya na Amir na Mbashiri Mkuu na bendera ya taifa ilipandishwa na Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mheshimiwa January Makamba. Katika ufunguzi Amir na Mbashiri Mkuu aliwasomea wahudhuriaji ujumbe muhimu uliotolewa na Khalifatul Masih V atba uliokumbusha kuwa Jalsa Salana si mkutano wa kidunia, maonyesho au tamasha. Lengo la Jalsa Salana ni kuoata ukaribu na Allah, kujiendeleza kielimu ya kiroho na kuleta mabadiliko maishani mwetu. Amir sahib alitoa rai kwa wahudhuriaji kusikiliza kwa makini hotuba zitakazotolewa, kutimiza masharti ya Baiat, kusikiliza hotuba za Ijumaa za Huzur bila kukosa na kufanya mahubiri ambayo ni moyo hasa wa Ahmadiyya.

Baada ya utangulizi huo wa kuwakaribisha wageni tokea Uingereza, Kanada, Uganda, Kenya, Malawi, Msumbiji, Amir alimkaribisha Mheshimiwa Makamba kuuhutubia mkusanyiko. Mheshimiwa Makamba alisisitizia jukumu la kuonyesha sura ya kweli ya Islam na akasema kazi hiyo imefanywa vizuri sana na Ahmadiyya. Makamba aliendelea kusema kuwa ni bahati mbaya sana ya kwamba picha halisi ya Islam imeharibiwa na kuchafuliwa na wale wanaojiita Waislamu kiasi hiki kwamba taswira ya Islam inahusishwa na ugaidi. Alisema ni jukumu la Waislamu kuondoa taswira hiyo mbaya na akaisifia sana kazi inayofanywa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ya kusafisha taswira iliyochafuliwa na wale wanaojiita Waislamu. Na katika siku ya mwisho ya Jalsa Salana, Waziri Mkuu - Mheshimiwa Kassim Majaliwa akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Dokta John Pombe Magufuli alitoa hotuba akiisifia Jamaat kwa mchango wake katika maendeleo ya kijamii na hasa ushiriki wa kindakindaki katika kustawisha amani. Waziri Mkuu alisema suala la amani ni muhimu sana nchini na ndio lenye kushika hatamu ya kila kitu nchini. Pia aliisifia kazi nzuri inayofanywa na Jamaat nchini.

Suala lingine la muhimu ni wanajumuiya kuweza kuchangia damu kwa benki ya damu ya taifa. Jalsa Salana 2017 ilihudhuriwa na wageni toka nchi jirani na za mbali akiwemo Amir na Mbashiri MKuu aliyepita - Sheikh Faiz Ahmad ambaye pia ni mkuu wa kitengo cha kufasiri Kiswahili MTA pamoja na wenyeji waliofikia zaidi ya elfu nne (4000).



Mh. January Makamba akihutubia wanajumuiya katika kikao cha kwanza cha mkutano wa Jalsa Salana 2017 ambapo alipata kualikwa kwa mara ya pili.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdulrahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Atangaza mwaka wa 84 wa Tahrik Jadid.

Kutoka uk. 1

Leo ningependa kuitoa katika njia ya Allah Mwenyezi." Hivyo ndivyo vilikuwa viwango vya Masahaba wa Mtukufu Mtume (saw).

Leo, kwa fadhila za Allah Mtukufu, ni wafuasi wa yule mtumishi mwenye shauku wa Mtukufu Mtume (saw) ambao wameelewa juu ya aina zote za kujitolea. Na ni Waahmadiyya ambao wamewazidi wengine kwa kuonyesha mfano katika hili. Leo, dunia imekamatwa katika mbio za kutafuta mali. Kuna idadi kubwa ya Waahmadiyya, ambao wanatafuta fedha, lakini wanapokumbushwa kuhusu kujitolea mali, wanatoa mali zao. Yote hii ni kutokana na elimu ya kiroho inayotolewa na mafunzo ambayo Masih Aliyeahidiwa (as) aliyotupatia. Hivyo, katika moja ya sehemu, ambayo Masih Aliyeahidiwa (as) alikuwa anazungumzia juu ya kujitolea mali, alisema: "Katika dunia, mwanadamu ana mapenzi makubwa na mali. Hii ndio maana imeandikwa katika tafsiri ya ndoto kuwa, ikiwa mtu ataona anatoa ini lake na anampatia mtu mwingine, inamaanisha atatoa mali.

Hii ndio maana ili kufikia Ucha Mungu wa kweli na imani, imeelezwa kuwa, "**Hamtoweza kuufikia wema hasa mpaka mtoe kile mnachokipenda**…" (3:93), kwa sababu sehemu kubwa ya utu na huruma juu ya viumbe vya Allah, inategemea kujitolea mali" Masihi Aliyeahidiwa (a.s) aliendelea kusema zaidi, "Huruma kwa wanadamu na viumbe wa Allah ni sehemu ya pili au ni nusu ya imani, bila ya hiyo imani haiwezi kuwa kamili na madhubuti."

Masih Aliyeahidiwa (as) alisema, "Kujitolea kwa Hadhrat Abu Bakar (ra) kwa ajili ya Allah Mwenyezi katika uhai wake kulikuwa ni kwa kiwango hiki na kulikostahili kiasi ya kwamba wakati Mtukufu Mtume (saw) alipoomba kujitolea kwa ajili ya dini, alijipeleka kwa Mtukufu Mtume (saw) na kila alichokimiliki."

Kama nilivyoeleza, kuna Waahmadiyya wengi, ambao wanafanya juhudi ili kufikia kiwango cha juu cha kujitolea mali. Wanaposoma Qurani tukufu, hadithi na pia maandiko ya Masih Aliyeahidiwa (as), wanapata imani madhubuti kuwa Allah Mwenyezi ametaja baraka kwenye mali na roho za wale waliojitolea katika njia ya Allah. Allah Mtukufu pia Alisema kuwa ikiwa mtu atatoa kile anachokipenda katika njia yake, Atamrudishia kikubwa zaidi, na kwa hakika, Anaweza Kumzidishia mara mia saba na zaidi ya hivyo.

Hivyo, Waahmadiyya wanapojitolea kwa kiasi hicho, wanakuwa na yakini pia kwamba Allah Mtukufu Atarudisha kwao mara nyingi zaidi na pia Atawatendea kwa njia ile ile. Waahmadiyya wanapotoa mali zao sawa na muongozo huu wa Mtukufu Mtume (saw) ambapo alisema yeyote anayejitolea hata tende moja katika njia ya Allah Mtukufu katika zile alizozitafuta kwa halali (*ni jambo la msingi kukumbuka kuwa Allah Mtukufu hapokei pato lisilo la halali, ambalo limepatikana kwa njia za udanganyifu, anapokea kitu kilichokuwa halali tu*), ataipokea tende hiyo kwa mkono wake wa kuume, hata kama atalinganisha mali hiyo na tende, Ataendelea kuiongeza hadi ifikie ukubwa wa mlima. Alisema kuwa hii ni kama yeyote miongoni mwenu anayemlisha ndama kuanzia udogo wake hadi anakuwa mnyama mkubwa.

Hivyo basi, tunaposoma na kusikiliza habari hizi na miongozo ya Mtukufu Mtume (saw) [tunatakiwa tukumbuke kuwa] hizi sio habari za watu waliopita. Bali, hali za watu kujitolea mali zinapatikana hata leo pia. Hivyo, nitawasilisha baadhi ya hizi habari.

Kutoka Cameroon, ambayo ni nchi ya Kiafrika, Mbashiri wetu anaeleza kuwa, kuna Mwalimu wa Jamaat, anaeitwa Abu Bakar sahib, ambae ameeleza kuna Ahmadiyya kwa jina la Abdullah, alikuwa hana ajira mwaka uliopita na alikuwa amekutana na hali ngumu kiasi hiki ya kwamba alishindwa kuisaidia na kuihudumia familia yake. Katika hali hii, siku moja alihudhuria sala ya Ijumaa na baada ya Sala ya Ijumaa, wakati katibu wa Tahrik Jadid alipotoa tangazo kuhusiana na Tahrik Jadid, Abdullah Sahib alikuwa na Franc elfu kumi mfukoni mwake. Pale tu aliposikia tangazo la Tahrik Jadid, alitoa fedha yake yote kwa ajili ya Tahrik Jadid. Siku chache baadae alirudi katika kituo cha sala na kusema Allah Mtukufu Amepokea mchango wangu. Ndani ya wiki moja kuna kampuni binafsi ilinipatia kazi na kuidhinisha mshahara wa Franc Laki moja, ambayo ni mara kumi zaidi ya mchango wangu.

Kuna Ahmadiyya mpya aliyejiunga, kwa jina la Daudi Sahib kutoka Congo Brazzaville, ambayo pia ni nchi ya Kiafrika. Kwa kuangalia hali yake ngumu ya uchumi, aliombwa awe anashiriki kila sala ya Ijumaa katika Msikiti wa Ahmadiyya. Alipoanza kuhudhuria sala za Ijumaa mara kwa mara, siku moja kwenye kikao cha faragha baada ya sala ya Ijumaa, alielezwa umuhimu wa kujitolea mali na alielezwa kuwa unatakiwa utoe kiasi kidogo katika kila kile Allah Mtukufu Alichokuruzuku katika njia yake. Wiki moja baadae, alikuja katika sala ya Ijumaa na alikuwa anaonekana mwenye furaha kubwa kufuatia Ijumaa ile.

Nilimuuliza kuhusiana na jambo hili, na alinieleza kuwa kufuatia msisitizo ulionipatia juu ya kulipa Chanda kwenye Ijumaa iliyopita, nilitoa Franc mia moja kwa ajili ya Chanda kabla ya kuondoka Msikitini. Baada ya kulipa mchango, punde tu nilipofika nyumbani, jirani yangu wa karibu ambae alihifadhi kuni katika bustani yangu kwa muda mrefu, alikuja kuchukua kuni zake na alinipatia kiasi cha Franc elfu nne wakati anaondoka. Nilikuwa na furaha sana kwamba nilipofika nyumbani baada ya kulipa Chanda na Allah Mtukufu papo hapo aliniongezea mara Arobaini zaidi na kunirudishia.

Hazur (atba) alisimulia matukio mengi ya kuongeza imani ambayo watu waliojitolea kifedha ingawa walikuwa na matatizo ya kifedha na Allah Mwenyezi Akawazawadia kwa wingi bila kuchelewa.

Mbashiri kutoka katika kisiwa cha Mayote anaandika kwamba Mayote ni nchi masikini sana ambako watu wanaishi kwa taabu kwa kuuza mbogamboga na kadhalika majumbani mwao. Rafiki mmoja Muahmadiyya, Rabyoon Sahib, anafanya kazi katika gereji ya pikipiki na anatoa chanda kubwa kuliko wote. Anasema kwamba ni ajabu kwamba kiasi chochote ninachokitoa kama chanda ninapata mara mbili ya kiasi hicho mwishoni mwa mwezi. Siku moja mke wake akamuuliza "Kwa nini unatoa Chanda kiasi chote hicho?" Akajibu: Mungu Mwenyezi Ananirejeshea mara mbili ndio maana ninatoa hivyo.

Kisha akatoa kiasi fulani mbele ya mke wake na akasema: "Uone jinsi Mungu Mwenyezi bila shaka Atakavyonirejeshea kiasi hiki". Kisha, hilo lilitimizwa wakati mwisho wa mwezi mmiliki wa duka alipowapa wafanyakazi wote bonasi na kiasi alichopokea kama bonasi kilikuwa ni kikubwa kuliko kile alicholipa katika Chanda.

Kwa Baraka za Allah, tokea Jumuiya imeanzishwa mpaka leo hii waaminio wameshuhudia matendo na ahadi za Mungu Mwenyezi. Nimesimulia matukio ya Waahmadiyya wa zamani, wa sasa na ya wanajumuiya wapya wengi. Sadaka zinazotolewa katika zama hizi, na hasa sadaka za kifedha ni sifa bainifu ya Jumuiya hii. Waahmadiyya wengi wanatambua kwamba zama hizi, ambazo ni zama za kukamilika kwa uenezi wa Islam, ambao kwao Mungu Mwenyezi Amemleta Masihi Aliyeahidiwa (as) na ambao unafanyika kwa kusambaza na kutafsiri Qur'ani Tukufu katika lugha mbalimbali, na kwa kueneza vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa (as), vitabu vya Jumuiya, kwa kujenga misikiti, kuanzisha nyumba za jumuiya, kuanzisha vyuo vya mafunzo ya dini ambapo leo hii tuna vyuo hivyo huko Asia, Afrika, Ulaya, Marekani ya Kaskazini na Indonesia ambako wabashiri wanahitimu kueneza ujumbe wa Islam, basi Waahmadiyya wanapoona mambo yote hayo, wanajua kwamba kuna haja ya kujitolea sadaka kifedha na kwa kweli wanajitolea sadaka kifedha.

Hii hasa ndio hali katika siku na zama za sasa pamoja na yale ambayo nimeisha yasema. Watu wanapotanabahishwa, basi watu wanazingatia. Hii ndio sababu niliposema tuongeze idadi ya washiriki katika Waqfu-e-Jadid na Tahrik-e-Jadid idadi sasa inaongezeka. Baada ya kuwataka wazingatie kuhusu hili hamu ya kujitolea sadaka imeonekana hata kwa watoto wa Kiahmadiyya. Hivyo, mbashiri wa Nakuru, Kenya anaandika kwamba Raisi wa sasa wa Jamaat, Abu Bakr Kibi Sahib ambaye ni Muahmadiyya mtiifu sana na anafanya kazi katika Jeshi la ulinzi la Kenya akiwa ni Sajenti, ingawa anaishi mbali na msikiti huko eneo la Cantonment, siku zote anasafiri safari ndefu ili kusali sala za Ijumaa na anakuja na mabinti wake watatu. Siku chache zilizopita baada ya sala ya Ijumaa alimwambia mbashiri kwamba binti yangu pia alisikia hotuba hii na katika mwezi huo mgeni mmoja alimtembelea nyumbani kwake. Wakati mgeni huyo anaondoka alitoa shilingi ishirini na tano kumpatia binti yangu mdogo kabisa ambaye alikuwa na miaka mitano wakati ule. Mgeni alipoondoka msichana huyu alimwendea baba yake na wakati akimpa shilingi ishirini alisema toa hizi kwenye Tahrik Jadid kwa ajili yangu na shilingi tano zilizobaki nitatumia kwa kitu fulani cha kula.

Hivyo, mifano hiyo ya kujitolea sadaka inaweza kuwa sifa bainifu ya Wahmadiyya tu, wadogo kwa wazee na wanaoishi popote pale duniani. Sadaka inayotolewa na mtoto kwa hakika ni mwangwi wa asili yao ya kiucha Mungu. Ninamuomba Mungu Mwenyezi Aiwezeshe Jamaat kuendelea kutoa watoto wa aina hiyo na wazee ambao wameingizwa hamu na hamasa ya kujitolea sadaka kwa ajili ya Mungu Mwenyezi na waendelee kutimiza ahadi zao walizozifanya.

Kama ilivyo desturi, mwaka mpya wa Tahrik Jadid unatangazwa mwezi Novemba na leo nitatangaza mwaka wa 84 wa Tahrik Jadid na pia nitatoa hali ilivyokuwa kitakwimu katika mwaka uliopita. Mwaka wa 83 wa Tahrik Jadid umefikia kikomo, na kama nilivyosema, mwaka wa 84 umeanza tarehe 1 Novemba. Sawa na ripoti ambazo zimewasilishwa mpaka sasa, Jamaat imewezeshwa kutoa jumla ya sadaka ya Paundi za Kiingereza milioni 12.58, Alhamdulillah, Sifa zote njema zinamhusu Allah. Kwa baraka za Mungu Mwenyezi, hili ni ongezeko la Paundi za Kiingereza milioni 1.57 kutoka makusanyo ya mwaka jana. Kwa kuangalia makusanyo ya jumla, kama tukiiweka nje Pakistani, Ujerumani ni namba moja. Namba mbili ni Uingereza, namba tatu ni Marekani, namba nne ni Kanada, namba tano ni India, namba sita ni Australia, namba saba ni Indonesia, namba nane ni Jamaat moja ya Mashariki ya kati, namba tisa pia ni Jamaat nyingine ya Mashariki ya Kati na Ghana ni ya kumi.

Kwa kuangalia makusanyo ya jumla kutoka nchi za Afrika, mafanikio ya kuonekana yako katika mfuatano ufuatao: Ghana, Nigeria, Mali, Cameroon, Liberia na kisha Benin.

Kwa vyovyote vile, jumla ya kiasi kinapatikana, hata hivyo katika miaka michache iliyopita nimekuwa nikisisitiza kuwaingiza watu wengi iwezekanavyo katika wachangiaji wa jumla. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: Chanda ni lazima ichukuliwe kutoka kwa kila mmoja, hata kama ni senti moja tu.

Muundo wa kiutawala kuhusiana na mikoa yao umebadilika kidogo huko Pakistani. Kwa hiyo, badala ya wilaya zao, orodha imeletwa kuhusiana na Jamaat zao kama ifuatavyo: Rabwah, Islamabad, Lahore Township, Azizabad Karachi, Delhi gate Lahore, Rawalpindi, Multan, Peshawar, Quetta na Gujranwala.

Kwa ngazi ya wilaya huko Pakistani hali iko kama ifuatavyo: Sargodha, Faisalabad, Umerkot, Gujrat, Narowal, Hyderabad, Mirpur Khas, Bhawalpur na Okara zimefungana, na kisha Toba Tek Singh na Kotli Azad Kashmir.

Jamaat kumi za mwanzo huko Ujerumani ni kama ifuatavyo: Neuss, Lindow mark, Main-Garten, Nidda, Domberg. Mehdi Abad, Heidelberg, Limburg, Kiel na Florsheim.

Kwa kuangalia mikoa yao, nafasi za kumi bora ni kama ifuatavyo: Hamburg, Frankfurt,

Endelea uk. 4

Atangaza mwaka wa 84 wa Tahrik Jadid.

Kutoka uk. 3

Morfelden, Gross-Gerau, Wiesbaden, Dietzenbach, Mannheim, Riedstadt, Darmstadt na Offenbach.

Jamaat kumi kubwa za kwanza katika Uingereza, kwa kuangalia michango, ni kama ifuatavyo: Masjid Fazl, Worcester Park, Birmingham South, Bradford South, Putney, Glassgow, Islamabad, New Malden, Gillingham, Scunthorpe.

Kuhusiana na hali ya mikoa kwa wastani wa mchango wa kila mtu ni kama ifuatavyo: South West, North East, Islamabad, Midlands na Scotland.

Nafasa za Jamaat huko Marekani ni kama ifuatavyo: Silicon Valley, Oshkosh, Seatle, Detroit, York, Los Angeles, Silver Spring, Central Jersey, Chicago South, West Antlantis, Los Angeles Inland.

Nafasi ya mikoa ya huko Canada kwa kuangalia makusanyo yao ni kama ifuatavyo: Vaughn, Peace village, Brampton, Vancouver na Mississauga.

Nafasi ya Jamaat huko India ni kama ifuatavyo: Kerala, Carnatic, Jammu Kashmir, Telangana, Tamil Nadu, Odisha, Punjab, Bengal, Delhi, Maharashtra.

Nafasi za jamaat kubwa huko India ni kama ifuatavyo: Calicut Kerala, Kathaprem Keral, Qadian, Hyserabad, Calcutta, Bangalore, Kenal Town, Pingadi, Matutum na Keroli.

Nafasi ya Jamaat huko Australia ni kama ifuatavyo: Castle Hill, Melbourne, Berwick, Canberra, Marsden Park, Brisbane, Logan, Adelaide South, Compton, Melbourne Longwarry. Pezith, Melbourne East.

Ninamuomba Allah Mwenyezi Ajaalie Baraka nyingi kwenye mapato yao na vizazi vyao. Amin.

Baada ya haya ninapenda kuzindua mpango mpya, ambao kimsingi ni kwa wale waishio Uingereza na pia uko wazi kwa watu wote wenye uwezo duniani; na (wito) huo ni kwa ajili ya kukarabati sehemu ya Msikiti wa Baitul Futuh iliyoungua takriban miaka miwili iliyopita. Tokea mwaka 1984 - na hasa katika mazingira ya sasa – kutokana na kuhamia kwa Ukhalifa, wanajumuiya kutoka sehemu zote za dunia wamekuwa wakija hapa na wanapatiwa malazi. Zaidi ya hayo kuna matukio mbalimbali ambayo yanafanyika hapa. Mpango wa ujenzi mpya umeisha kamilika na kiasi kinachohitajika ni kikubwa kwa mbali kuliko hapo kabla. Ingawa eneo ni kubwa kidogo tu kuliko lilivyokuwa, makadirio ya jumla ni makubwa hasa.

Mpango mpya uliopendekezwa pia utagharimu takriban paundi za Uingereza milioni 11. Kati ya hizo takriban nusu zimepatikana kutoka Bima na pia baadhi ya watu wamechangia. Hata hivyo, zaidi kidogo ya nusu ya kiasi hicho bado kinahitajika na kwa kiasi hicho watu watalazimika kujitolea sadaka, kama ambavyo daima wamekuwa wakifanya hivyo.

Katika tukio moja Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema: "Wakati wa ufalme wa Alamgir, Msikiti wa Kifalme uliungua moto. Watu wakaja mbio na kumueleza mfalme kuhusiana na moto huo. Aliposikia hilo mfalme akaanguka kusujudu akitoa shukrani zake. Mawaziri wakashangazwa na hilo na wakauliza: 'Ewe Mkuu! Unawezaje kuonyesha shukurani wakati nyumba ya Mungu inaungua, jambo ambalo limeifanya mioyo ya Waislamu kutokwa damu" Kwa hilo Mfalme akajibu: Umri umepita ambamo nimekuwa natafakari kuhusu msikiti huu mtakatifu na jinsi jengo hili lilivyowafaidisha maelfu ya watu. Nilikuwa nikisema kama kungepatikana fursa tu ya mimi kushiriki katika mpango huu wa thamani na mtukufu. Lakini, nililiangalia jengo kutoka katika kila pembe na kuliona kuwa limekamilika na halina ufa wowote wa aina yoyote. Sikujua ni jinsi gani ninaweza kupata zawadi kutokana na huo. Hivyo, leo, Mungu Mwenyezi Amenifungulia njia ambayo kwayo ninaweza kuzipata Baraka. Na Mungu Mwenyezi ni Msikivu, Mjuzi."

Hivyo, kama nilivyosema hapo kabla, wale watu ambao hawakuweza kujitolea sadaka kwa ajili hii hapo kabla ni lazima wafanye jitihada kushiriki safari hii. Ni lazima wajaribu kulipa kiasi walichoahidi ndani ya miaka mitatu na wajitahidi kulipa moja ya tatu ya ahadi zao ndani ya mwaka wa kwanza.

Baada ya sala nitaongoza sala ya jeneza ghaib ya Bwana Adil Hamooz Nakhooza Sahib kutoka Yemen. Amefariki tarehe 14 Oktoba kutokana na moyo kushindwa kufanya kazi akiwa na umri wa miaka arobaini. *Inna lillahi wa inna ilaihi raajiuun.* Mwanajumuia mwenye jina la Ali Arghami Sahib anaeleza: "Marehemu alikuwa akiwakaribisha baadhi ya marafiki nyumbani kwake nikiwemo na mimi na alikuwa akiulizia kuhusu Ahmadiyyat. Tulikuwa tukimueleza kuhusu masuala mbalimbali yanayobishaniwa kama vile kutokea kwa mpinga Kristo, maisha na kifo cha Masihi (Isa as) na pia kutokea kwa Mahdi. Marehemu ameacha mjane, mtoto mmoja wa kiume na binti mmoja.

Ninamuomba Allah Ainue cheo cha marehemu, Amsamehe na Ammiminie Baraka kwa kumjaalia makao miongoni mwa wapendwa wa Mungu. Amin. Ninamuomba Amlinde na Amsaidie mke wake na watoto na pia Awajaalie kila haja yao. Ninamuomba Awawezeshe kuwa wacha Mungu na waadilifu na Awawezeshe kufuata nyayo za baba yao. Amin

UJUMBE WA JALSA SALANA TANZANIA 2017 KUTOKA KWA HADHRAT KHALIFATUL MASIH WA TANO (ATBA)

Wapendwa Wanajumuiya wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania

Assalaam alaikum warahmatullah wabarakaatuh.

Nimefurahishwa sana kwamba mnafanya Jalsa Salana yenu tarehe 29 na 30 Septemba mpaka tarehe 1 Oktoba 2017. Dua niombayo ni kwamba Allah Aibariki Jalsa yenu ipate mafanikio makubwa na washiriki wote wapate baraka nyingi za kiroho kwa kushiriki mkusanyiko huu wa kipekee wa kiroho na nyote daima muendelee kusonga mbele katika wema wa nyoyo, ucha Mungu na kufanya matendo mema.

Daima msiache kukumbuka kwamba Jalsa Salana ya Jamaat Ahmadiyya sio tukio la kawaida la kidunia au maonesho au starehe. Kusudio lake ni moja tu kwamba wanajumuiya wapate ukaribu na Allah, waongeze elimu yao ya dini na uelewa, kuleta mabadiliko mema katika maisha yenu na kuyafanya yawe sehemu ya maisha yenu ya kawaida; kuwalinda na tamaa na mvuto wa maisha haya yapitayo, kuchochea mahusiano ya mapenzi, huba na udugu baina ya wanajamaat na kati yetu na binadamu wenzetu wote, kufanya jitihada ya kutimiza majukumu haya adhimu kwa uwezo na vipawa vyetu vyote, na hatimaye tuhakikishe kwa nia thabiti tunaeneza ujumbe wa amani wa Islamu kwenye kila pembe ya ardhi.

Sikilizeni kwa makini hotuba za wanazuoni mbalimbali wa Jamaat. Kama nilivyosema katika Jalsa ya karibuni ya Jamaat ya Uingereza, jaribuni kuelewa na kunufaika kutokana na nukta nyingi za kiroho na kielimu zinazotajwa katika hotuba hizo. Wasemaji wameweka juhudi kubwa katika kuandaa mada zao kwa hiyo ni muhimu kuwasikiliza vizuri. Kwa hivyo hudhurieni Jalsa kwa uaminifu wa moyo na kwa nia ya kutekeleza mtakayo jifunza. Ni rehema maalum ya Allah juu yetu kwamba wanazuoni wetu huneemeshwa kwa maneno ya Allah, Mtume Wake s.a.w. na Masihi Aliyeahidiwa a.s. na kuwasilisha elimu hiyo kwetu.

Ikiwa tutatekeleza mafundisho yao hayo, tunaweza kuleta mapinduzi makubwa ya kiroho. Allah Awawezeshe wahudhuriaji wote wa Jalsa kutimiza malengo na makusudio yake.

Ninawahimiza nyote mjidhatiti kutimiza masharti ya baiat zenu na hususan kuienzi taasisi ya kiroho ya Khilafat - e - Ahmadiyya. Jueni ya kwamba maendeleo ya Jamaat, kuenea kwa Islam na kwa hakika kupatikana kwa amani duniani, kimsingi vimeambatana na taasisi ya Ukhalifa.

Kwa hiyo, ninawaomba wanajumuiya wa Jamaat ya Tanzania daima kubakia waaminifu na watiifu kwa Ukhalifa. La muhimu kabisa, yawapasa kuwaeleza watoto wenu baraka za kipekee za Khilafat - e - Ahmadiyya na kuwahimiza wabaki wameungana nayo. Waiombee taasisi hii na wadumu katika utii kwa Khalifa wa zama.

Siku zote sikilizeni hotuba zangu za Ijumaa, vizuri zaidi kupitia matangazo mubashara (live) na mada na hotuba zangu katika shughuli na matukio mengine ya muhimu. Sasa tunabarikiwa kwa kuwa na idhaa (channel) ya MTA Afrika kwa hiyo nawahimizeni muangalie MTA mara kwa mara na kadhalika muwahimize wanafamilia wenu, hususan watoto wenu, kufanya hivyo pia. Kwa kuangalia vipindi vingi mbalimbali vya MTA ufahamu wenu wa uzuri wa Islam na ukweli wa Ahmadiyyat utaongezeka na kuimarika sana.

Mkiwa ni wanachama wa Jumuiya ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. mnabidika daima kuenenda sawa na mafundisho yake kwa kujipambanua vyema kama wanajumuiya waaminifu na wema katika mambo yenu yote na matendo na hasa kwa kuwa wakarimu, wanaothamini na kujali wengine. Zaidi ya hayo muwe ni mfano mwema kwa tabia na muwe raia wema na muonyeshe uzalendo kwa taifa lenu, hii ni kwa sababu ni fundisho la msingi la Mtume wetu s.a.w. kwamba "Mtu kupenda nchi yake ni sehemu ya imani".

Ville vile napenda kuwakumbusheni juu ya wajibu wenu kuhusiana na mahubiri ambayo ni faradhi kwa kila Ahmadiyya na wakati wote tafuteni mikakati mipya ya kuondoa upotoshwaji dhidi ya Islam, na kueneza ujumbe wa Amani wa Ahmadiyya katika nchi yote ya Tanzania na Afrika Mashariki,

Allah Aibariki Jalsa yenu kwa kila mafanikio na kuwawezesheni nyote kupata nafasi ya kuendelea sana katika taqwa (Uchamungu) na maendeleo ya kiroho. Allah Awawezeshe kuleta mapinduzi ya kiroho katika maisha yenu kuelekea uchamungu, mwenendo mwema na kuwatumikia binadamu na awafanyeni muwe wachangiaji wa mfano katika kuleta amani duniani.

Allah Awabarikini nyote.

Wassalaam

Wenu Mwaminifu

Imesainiwa

MIRZA MASROOR AHMAD
KHALIFATUL MASIH V

Msiba wa Bwana Ali Saidi Mosse

Na Sheikh Yusuf Kambaulaya, Songea

Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. aliagiza kwa kila Muislamu kufanya juhudi za kumtambua Imamu wa zama zake. Akasema kuwa yule asiyemtambua Imamu wa zama zake, basi huyo amekufa kifo cha kijahili. Yaani anakuwa anaishi maisha ya kutotambua baraka za kiongozi wake wa kiroho wa zama zake. Huu ni wajibu wa kila Muislamu kuhakikisha anamtafuta ili anapofanikiwa kumtambua basi ajiunge naye na amtii kila amri yake njema.

Miongoni mwa watu wenye bahati njema ya kumtambua Imamu wa zama zetu ni marehemu Bw. Ali Saidi Mosse ambaye baada ya kuhubiriwa na mjomba wake marehemu mzee Saidi Khatibu akaanza kufanya uchunguzi juu ya ukweli wa madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masih, Imamu na Mjumbe wa zama zetu hizi.

Baada ya kuridhika na madai yote ya mjumbe huyu wa Allah akaamua kujiunga na Jamaat ya Waislam Waahmadiyya, na Bw.. Ali Saidi Mosse alidumu katika imani yake hiyo mpaka alipofikwa na mauti tarehe 30/09/2017 ; *Inna Lillahi wainnaa ilaihi rajiuun*. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

Kwa mara ya kwanza kabisa mimi nilikutana na marehemu Bw. Ali Saidi Mosse katika msikiti wa Jamaat Ahmadiyya Tanga mwaka 1973 wakati mimi nikiwa Mbashiri na yeye alikuwa anamaliza masomo yake ya High School katika Shule moja Tanga Mjini.

Marehemu Shekhe Abu Talib Iddi Sandi akanitambulisha kwa Bw. Ali Saidi Mosse kuwa huyu ni Ahmadiyya mwanafunzi hodari na ni mwenye Imani thabiti sana. Yeye marehemu Bw. Ali Saidi Mosse sawa na nafasi yake alikuwa anafika msikitini siku ya Ijumaa kwa ajili ya sala za Ijumaa na kama kulikuwapo na shughuli yoyote muhimu alikuwa akijitahidi kufikia msikitini kwa ajili ya shughuli hiyo.

Katika nyakati zingine pia alikuwa anaonesha kupenda Jamaat na alikuwa anajitahidi kuelezea kwa lugha fasaha iliyowavutia sana wanafunzi wenzake. Alikuwa akiwaleta baadhi ya rafiki zake waje wajionee wenyewe taratibu za ibada zetu na wapate fafanuzi juu ya maswala mbalimbali waliyohitaji wayaelewe zaidi.

Kwenye miaka ya sabini mwishoni marehemu Bw. Mosse alihamia Tabora akiwa anafanya kazi katika benki ya N.B.C. Alipokuwa Tabora alikuwa anashiriki kikamilifu katika shughuli zote za Jamaat Ahmadiyya mkoani Tabora. Katika nyanja za mahubiri alikuwa mstari wa mbele na alikuwa amejaaliwa kipaji cha kuongea lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha na hoja alizokitoa ziliwafanya wasikilizaji wake waathirike sana, baadae Bw. Ali Saidi Mosse alikwenda Uingereza kwa ajili ya masomo ya Juu aliporejea akaendelea na kazi serikalini.

Katika safari yake moja alitembelea Songea, safari hii ilikuwa inamfanya akae hapa zaid ya wiki tatu hivi. Jioni moja alipofika msikitini nikamshauri mara



Bwana Ali Saidi Mosse 1950 – 2017

nyingi kufikia nyumba za wageni huwa mtu hapati nafasi za kufanya ibada kwa utulivu, unaonaje uje upumzike katika nyumba ya Jamaat ina nafasi na pia utapata fursa njema za kufanya ibada kwa utulivu; Bw Mosse akaafikiana na ushauri wangu na siku ya pili yake akahamia nyumba ya Jamaat, tukakaa nae kwa amani na utulivu mpaka alipo ondoka kurejea Dar.

Nikiwa Dodoma, Bw. Ali Saidi Mosse alikuja hapo akifuatana na wataalam wenzake kwenye bunge la Bajeti na alikuwa na uhuru wa kukaa popote alipopenda. Kwanza alifikia hotelini na baada ya kuonana nikamshauri mara hii tena kuja kukaa katika nyumba ya Jamaat, nae akakubali, akaja tukakaa nae mpaka alipomaliza shughuli zilizomleta akarejea Dar kwa amani na furaha.

ATEULIWA KUWA AMIRI JAMAAT

Hadharat Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masihi wa tano a.t.b.a. alizuru Tanzania mwaka 2005 na muda mfupi baada ya kurejea London Uingereza tukapata taarifa kuwa Huzur a.t.b.a. amefanya uteuzi wa Amir mpya kwa Tanzania na kwa bahati mzuri Bw. Ali Saidi Mosse ndie ameteuliwa kuwa Amir Jamaat wa kwanza mzawa wa nchi hii sote tukamshukuru sana Huzur kwa uteuzi huu, na pia tukamuombea Bw. Mosse Allah Amsaidie sana na Amjalie busara, hekima, huruma, na uongozi bora. Kufuatia uteuzi huu marehemu Bw. Ali Saidi Mosse alifanya kazi za uamiri kwa bidii na akawa amejitolea kwa maisha yake yote kuitumikia Jamaat usiku na mchana.

Katika kipindi chake alifanya kazi ya kuendeleza Jamaati zote katika Nyanja zote. Akaandaa semina katika mikoa yote ambayo yeye mwenyewe alisaidizana na Alhaji Sheikh Abdulrahman Ame na Mwalim Omari Mnungu. Semina hizi zilisaidia sana kuwaelewesha wanajamati taratibu nyingi za uendeshaji wa vikao vya Jamaat na hasa juu ya utoaji wa michango yote ya Jamaat Ahmadiyya.

Marehem Bw. Ali Saidi Mosse alikuwa muongeaji mzuri sana, hasa katika mikutano na hadhara mbalimbali. Katika Mji wa kibiti mkutano mmoja wa amani uliandaliwa na Jamaat. Mbali na Bw. Mosse viongozi wengine wa dini nao waliongelea mada zao lakini msemaji mkuu wa mkutano huo marehemu Bw. Mosse aliposimama na kuanza kuhutubia wasikilizaji wote walishangaa kuona mtiririko wa maneno na hoja zilivyokuwa vinaelezwa na marehemu, wote walipigwa na butwaa na hata alipomaliza hotuba yake mwenyekiti mwalikwa wa mkutano huo, Mkuu wa Wilaya mstaafu wa wakati huo Bw. Henry, akasimama na kusema kuwa kama elimu ya Islam ndiyo hii basi duniani hakuwezi kutokea dhuluma na mauaji na kila msikilizaji alitoka pale akitafakari kuwa viongozi wote Waislam wangehubiri kwa hali kama hii, bila shaka amani ingetawala duniani.

Kwa miaka miwili mitatu iliyopita marehemu Bw. Ali Mosse alifika Songea na Nyasa ambako alikuwa anawaelimisha hususan wanajamati na watu wengine jinsi ya kiondokana na umasikini kwa njia ya ufugaji wa kuku, watu wengi walinufaika na utaalam wake na wanaendelea kutumia utaalam huo kujiongezea kipato. Sambamba na utaalam huo wa kuwasaidia watu kujiongezea kipato marehemu Bw. Ali Saidi Mosse alikuwa amekerwa sana na maradhi yanayokabiliwa na jamii ya Kitanzania, hivyo basi akatuletea tiba ya magonjwa mbalimbali yanayotusibu ambayo tiba zake hupatikana kwa nadra na halafu ni ghali sana.

Tiba aliyotuletea huku ilikuwa ni mashine inayoitwa CERAGEM. Mashine hii watu wengi waliitumia, miongoni mwao wako waliosema kuwa wamepata nafuu na wapo wengine wanasema wenyewe kuwa wamepona kabisa. Kuna wengine walikuwa wanasumbuliwa na virusi ambao ndio waliosema wamepona kabisa na baadhi yao walidai kupona walikuwa wanasumbuliwa vidonda vya tumbo. Mashine hii baadae aliacha kwa dada yake hapo Bomba Mbili Songea na wakati ninajiandaa kuja Dar kwa ajili ya Jalsa Salana ya mwaka huu shemeji yake Bw. Ali Saidi Mosse aitwae Bw. Namwigo alileta mashine hiyo ofisini kwa maagizo ya marehemu tuweze kumpelekea Dar, na tulipeleka na kumkabidhi Bw. Jafari Mangoma ambae alipokea usiku wa Ijumaa kuamkia siku ya Jumamosi siku ambayo ndugu yetu Bw. Ali Saidi Mosse alifariki dunia.

Tunamuomba Allah Mwenye huruma Aipokee roho yake na Amuweke mahali pema peponi, na Awajaalie wanafamilia wake uvumilivu nao wawe ni warithi wema wa kuendeleza mema yote ya marehemu Bw. Ali Saidi Mosse. Amiin

TANZIA

Mzee Sultan Mohammed Ungando ametutoka

Wakati tunakwenda mtamboni kwa ajili ya uchapishaji wa toleo hili, tumepokea taarifa za kuhuzunisha kwamba mzee wetu, Sultan Mohammed Ungando, amefariki dunia. *Innaa Lillaahi wainnaa Ilayhi Raajiuun.* Sisi ni wa Allah na sote Kwake tutarejea.

Mzee Sultan Ungando amefariki dunia siku ya Ijumaa tarehe 8/12/2017 majira ya saa tatu usiku na kuzikwa siku ya Jumamosi tarehe 9/12/2017 katika makaburi ya Jamaat yaliyopo Wailes, Temeke Dar es Salaam.

Mbali na kuwa miongoni mwa Wanajamat wa mwanzoni nchini mwetu, mzee Sultan Ungando atakumbukwa kwa michango yake kadhaa aliyojitolea ndani ya Jamaat ikiwemo kutoa eneo lipatalo ekari tano huko Kitonga ambalo baadae likawa sababu ya kupata eneo kubwa zaidi linalotumika kwa ajili ya Jalsa Salana na Shule ya Ahmadiyya Sekondari.

Tunamuomba Allah Apokee kujitolea kwako huko na Amlipe malipo mema, peponi Amin.

Habari zaidi kuhusu maisha ya Mzee Sultan Ungando zitaandikwa kwenye toleo lijalo. *Inshallah*.

Bustani ya Washairi

MOSSE UMETANGULIA

1. Kwa jina lako Qayyumu, bwana kungwi naongea,
   Natamka kwa kalamu, kinywa kimenyong'onyea,
   Sote ni wake Karimu, na kwake tutarejea,
   Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

2. Kwenye Jalsa Salana, sote tulohudhuria,
   Tulihuzunika sana, pindi tuliposikia,
   Mose hatunaye tena, kwamba ameshajifia,
   Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

3. Ali Mose umekwenda, Akhera metangulia,
   Ingawa tulikupenda, Manani katuzidia,
   Uendako hutakonda, peponi utaingia,
   Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

4. Tulitamani ubaki, nasi katika dunia,
   Uzidi kimo na maki, umri kupindukia,
   Ila Mola mwenye haki, nani wa kumpangia?
   Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

5. Tulio sahibu zako, upweke tutapitia,
   Kuliziba pengo lako, vigumu itatuwia,
   Vipaji aina yako, ni haba kuinukia,
   Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

6. Wewe ulikuwa mwanga, njia kutuonyeshea,
   Jina jema umejenga, katika kujitolea,
   Ni mfano wa kuiga, kwa dini kuitetea,
   Mose umetangulia, Daima utakumbukwa.

7. Ni msomi mzamili, mchumi ulobobea,
   Kizungu na Kiswahili, Fasaha uliongea,
   Na kwa falsafa kali, hoja ulitujengea,
   Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

8. Kwa utunzi wa vitabu, Mose haukusinzia,
   Miradi ulikutubu, ya mali kujasiria,
   Mengi uliyaratibu, na ukayasimamia,
   Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

9. Kwa fadhili za Molao, kubwa umetuachia,
   Tafsiri ya Kiyao, ya neno lake Jalia,
   Wengi waipitiao, itawaongoza njia,
   Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

10. Ulipokuwa Amiri, wa kwanza Mtanzania,
    Matawi yalishamiri, nguvu yakajipatia,
    Jamati ikanawiri, ikawa inavutia,
    Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

11. Zile kumbi za kukodi, mikutano kufanyia,
    Zilikukera fuadi, na haukuvumilia,
    Ukafanya makusudi, Kitonga tukahamia,
    Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

12. Na sekondari Kitonga, ni wewe ulipania,
    Ukaapa tutajenga, na hilo likatimia,
    Leo nyoyo zinakonga, shule tunajivunia,
    Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

13. Ule wako ujasiri, wa nidhamu kukazia,
    Hata walio viburi, kugoma walihofia,
    Baadaye wakakiri, na heshima wakatia,
    Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

14. Hata zetu tanzimu, hamasa ulizitia,
    Ukaziongea hamu, ya mema kushindania,
    Japo kwa mwingi ugumu, malengo zilifikia,
    Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

15. Na ulipoamriwa, madaraka kuachia,
    Hukuwa mtu wa nongwa, ulijipumzikia,
    Na kamwe haukukwazwa, kutii walofatia,
    Mose umetangulia, daima utakumbukwa.

Abdullah Hamisi Mbanga (Kungwi)
Tambani, Mkuranga, Pwani

CHE MOSSE KATANGULIA (1950 – 2017)

Na Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)

1. Bismillahi Rahmaani
   Rahimu Mola Manani
   Kila kitu duniani
   Ni kwako kimeanzia.

2. Kila unachokiona
   Hata usichokiona
   Vyote ni vyako Rabana
   Na kwako vimetokea.

3. Kwa Jinalo nabutadi
   Ya Rabi Mola Wadudi
   Nilitimize kusudi
   Hili nilokusudia.

4. Kila kitu ni kwa nia
   Ndipo wakibarikia
   Kula amali binnia
   Kasisitiza Rasua.

5. Nia yangu kueleza
   Mosse alotekeleza
   Kwa juhudi akaweza
   Mola kamsaidia.

6. Na kampa msaada
   Umeleta matilaba
   Nao wingi wa faida
   Wa sisi kuendelea.

7. Sisi sote mashahidi
   Kwa ile yake juhudi
   Alofanya tufaidi
   Tunda la kujitolea.

8. Bila ya wewe hakuna
   Linaloweza kufana
   Au k uwa la maana
   Usipolibarikia.

9. Ni baraka za Rabana
   Ndipo kitu kinafana
   Bila hivyo ni laana
   Utajavua mabua

10. Naomba zako baraka
    Makusudi kunyooka
    Ili niweze kufika
    Kwa kuzipiga hatua.

11. Bila ya wako msada
    Msaada wa ziada
    Viumbe hatuna rada
    Ni rahisi kupotea.

12. Najikinga kwa Mkwasi
    Mola wa sisi inasi
    Wale walio wakwasi
    Na wengine fukaraa.

13. Ni wewe twakuabudu
    Waliobaki vibudu
    Ni wewe Mola Samadu
    Kwako tunaangukia.

14. Tutoe katika shari
    Zile nyingi hatari
    Za aendae kwa siri
    Ili tupate potea.

15. Kuweka wasi moyoni
    Kwa watu hata majini
    Tuepushe ya Manani
    Wajao kuangamia.

16. Kama Ulivyohubiri
    Zino siku za hatari
    Bila ya wewe Kahari
    Ni rahisi kupotea.

17. Uibariki safari
    Nitunge yenye nadhari
    Ya kupendeza Kahari
    Hayo ninayoyatoa.

18. Ukiridhi wewe basi
    Mletaji wa nemsi
    Ni wewe Mola Mkwasi
    Naomba yako ridhaa.

19. Bila ya Mola jalia
    Ni sahali kupotea
    Kulubaluba na njia
    Bila lengo kufikia.

20. Niongoze ya Rabuka
    Siratu ilonyooka
    Ili niweze kufika
    Nilipo kudhamiria.

21. Ulitakalo hutimu
    Chungu likawa ni tamu
    Wa mbele kuwa makamu
    Na nyuma akabakia.

22. Wamba kuni faya kuni
    Halikawi asilani
    Ulitakalo Manani
    Haraka linatokea.

23. Mfano wako hakuna
    Awezaye kufanana
    Jambo hili ni bayana
    Ni ukweli natongoa.

24. Bila ya wako msaada.
    Huwezi eleza mada
    Nipe nguvu za ziada
    Shabaha kuifikia.

25. Rabbishrahli swadri
    Wayassirli amri
    Ulimi uwe sukari
    Matamu ninayotoa.

26. Bila ya kulipitisha
    Hutofaulu maisha
    Hatima ni kuzamisha
    Yote ulojipangia

27. Kupanga neno ni nani
    Pasi na yako idhini
    Ufaulu asilani
    Asipopenda Jalia.

28. Ulitakalo ni sawa
    Tena ndilo sawasawa
    Bila yako majaliwa
    Haitaweza tokea.

29. Kwako ninanyenyekea
    Kwa upole na khushua
    Nakuomba ya Jalia
    Kwako ninategemea.

30. Kwako Rabbi nasujudu
    Ya Rabbi Mola samadu
    Si wawili ni wahadu
    Shahada ninaitoa.

31. Naomba chako kibali
    Niseme yalo asali
    Maneno yenye adili
    Mazuri kuyasikia.

32. Niseme yenye hekima
    Yaliyojaa uzima
    Tupate nasi kusoma
    Kwa ile yake tabia.

33. Maisha ya mwaminio
    Ninakushika sikio
    Kitu hicho ni kioo
    Chuo cha kujifunzia.

34. Kusoma kuelimika
    Ili upate ongoka
    Kutoichupa mipaka
    Rabbi alotuwekea.

35. Yalo mema kuyabeba
    Akina baba na mama
    Kweli ikawa ni tiba
    Maradhi kuyaondoa

36. Hayo tunayoeleza
    Si vizuri kuyabeza
    Busara kuyatimiza
    Mazuri tulogundua.

37. Neno lote la hekima
    Usikose kulichuma
    Ulichume himahima
    Ni mali ilopotea

38. Ni mali ya mwaminio
    Iliyozama machweo
    Irudi kwenye kituo
    Na kazi kuifanyia.

39. Sasa natoa salamu
    Kwa mpenzi wa kudumu
    Muhammad muungamu
    Khatama wa manabia

40. Wasalatu wa salamu
    Zimshukie Hashimu
    Alotumwa na Karimu
    Umati kutuokoa.

41. Kiongozi mtukufu
    Kiongozi ashirafu
    Sina budi kumsifu
    Amini Mustafaa

42. Roho inabubujika
    Mapenzi yasosemeka
    Kiumbe kakamilika
    Kazidi wote jamia.

43. Kwa usafi hata shani
    Kawazidi kwa thamani
    Tumwa wote wa Manani
    Ni yeye katangulia.

44. Amezidi ukaribu
    Karibu yake Wahabu
    Kwa matendo ya thawabu
    Ya huduma pamwe dua.

45. Hata uzuri kazidi
    Uzuriwe wa jasadi
    Mithili yake waridi
    Pale linapochanua.

46. Kila anapotamka
    Ni hekima inatoka
    Maneno yenye baraka
    Nao wingi wa usia.

47. Ndiye siraji muniri
    Ametangaza Kahari
    Kama tunataka nuri
    Muhammad ndiye taa.

48. Wale wapenzi wa Mungu
    Wa hivi sasa na tangu
    Kwa baraka za kimbingu
    Wote amewazidia.

49. Maji palipo na kiu
    Na wanyonge kuwa juu
    Analo daraja kuu
    Rehema katupatia.

50. Palipokuwa na vita
    Nao wingi wa kusuta
    Hivyo vyote alifuta
    Amani ikaenea.

51. Akaiwasha kurunzi
    Ikawaka ya mapenzi
    Na kutoweka simanzi
    Nyoyo zao kutulia.

52. Kashushiwa muujiza
    Watu tusije teleza
    Bileshi kujiumiza
    Kwa maasi kutokea.

53. Kitabu cha Qur'ani
    Muujiza duniani
    Mtunzi wake ni nani?
    Kama unamtambua!

54. Nieleze kwa makini
    Anatoka nchi gani
    Sisi tulo ujingani
    Nasi tupate kujua.

55. Tunasubiri kwa hamu
    Hilo tuweze fahamu
    Mtunzi huyo adhimu
    Kitabu kutuletea.

56. Ukweli ulo bayana
    Kateremsha Rabana
    Mola asiye na mwana
    Na kamwe hawezi zaa.

57. Kaeleza pasi shaka
    Mimi ni Mola Rabuka
    Mjuzi yote hakika
    Ni Mbora wa kujua.

58. Kitabu hakina shaka
    Kino kimeteremka
    Ili kije kutumika
    Kwa wamchao Jalia.

59. Ni Huda ilonyooka
    Isoweza kupindika
    Watu waweze kuvuka
    Peponi wende tulia.

60. Na kama wewe wabisha
    Aya moja jaribisha
    Uweze ipa maisha
    Ili iweze pumua.

61. Hai hati hai hata!
    Utabakia kujuta
    Bure wajipa matata
    Kitu kutoambulia.

62. Tambo ni hii yatamba
    Jitome kama ni mwamba
    Uone takavyo vimba
    Na siha kukupotea.

63. Kitabu kitakatifu
    Kutoka kwake Raufu
    Ndio huo msahafu
    Hazina isopungua.

64. Qur'an kwetu kaaba
    Twaizunguka kwa huba
    Tena kwetu ni katiba
    Ilosheheni sheria.

65. Kitabu kisicho shaka
    Tena kimekamilika
    Kila neno la Rabuka
    Nani wa kukibishia.

66. Kitabu kitakatifu
    Chenye mafunzo shufufu
    Kutukataza uchafu
    Na mema kusimulia.

67. Qur'an nadharia
    Vitendo ni vya Nabia
    Yeye kaifafanua
    Mtekelezaji sawia.

68. Kumbu kumbu Mustafa
    Bi. Asha kampa sifa
    Sururi na yake dhifa
    Mafunzo kuzingatia.

69. Hakuna alosaliza
    Bila kulitekeleza
    Yote ameyatimiza
    Bila ya kupata doa.

70. Maisha yake kitabu
    Soma utapata jibu
    Hakuna lilighibu
    Ya kwamba hakupitia.

71. Yeye ni mfano mwema
    Kufuata ni lazima
    Ili upate neema
    Toka kwa Mola Jalia.

72. Pia natuma salamu
    Zishuke kwa muadhamu
    Ahmad akramu
    Nabii pasi sheria.

CHE MOSSE KATANGULIA (1950 – 2017)

73. Ndiye Nabii buruzi
Kivuli chake azizi
Katu hanao ujuzi
Yeye kujitegemea.

74. Kupata hiyo nafasi
Alopewa na Qudusi
Kauza yake nafusi
Mtume kutumikia.

75. Mtumishi naye bwana
Hawawezi kufanana
Hilo kaweka bayana
Masingizio ondoa.

76. Na nuru hiyo ya mwezi
Chimbuko lake ni wazi
Jua ndio lenye kazi
Mwezi kuuangazia.

77. Bila jua huna mwanga
Ubaki kutangatanga
Kwenye giza umetinga
Vipi utajiopoa

78. Shamsi ni Muhammadi
Qamari ndiye Mahadi
Wametumwa na Wadudi
Kuifungua pazia.

79. Bila yeye Muhammadi
Asingekuwa Mahadi
Ni kwa huba na madadi
Mapenzi yalo kolea.

80. Naye Masihi Mauudi
Ni mwanae Muhammadi
Amefika kwa ahadi
Hashimu alotongoa.

81. Rehema nazo baraka
Kwake ziweze kushuka
Apate nae fanaka
Kwa njia ya buruzia.

82. Bila yake Muhammad
Huwezi kupata sudi
Ya kupata umahadi
Pasi kwake kupitia.

83. Ndiye yule akherini
Wa kurejesha imani
Hata iwe mawinguni
Chini atatuletea.

84. Ni kizazi cha Farisi
Alokuwa mfuasi
Huyo pasi wasiwasi
Imani katuletea.

85. Na ukiwa Muumini
Sikia yake maoni
Alotoa vitabuni
Na watu kuhutubia.

86. Na ukiwa unadhani
Mimi mtu wa shetani
(*Mungu Apishe mbali*)
Unitoe duniani
Wengi wasije potea.

87. Na kama hino Jamati
Si Jamati hasanati
Uipige kiberiti
Iweze kuteketea.

88. Na kama Umenituma
Kwa ujumbe wa rehema
Nizidishie neema
Wapate kunipokea.

89. Kama mimi ni Rasuli
Kutoka Kwako Jalali
Wafanye waone kweli
Matusi wanayotoa.

90. Kama kupenda bashiri
Huo ndio ukafiri
Basi mimi nakithiri
Ni kafiri kuzidia.

91. Kuisha utangulizi
Mwenzenu nina matozi
Ametawafu mjuzi
Rafiki wa kusifia.

92. Hae!Yadondokamachozi
Hae! Msiba mzito
Roho inawaka moto
La kufanya sijajua.

93. Kweli kitu mazoea
Kina tabu na udhia
Mtu ulomzoea
Mara ametangulia.

94. Kweli sasa naamini
Kuachana ni kanuni
Si leo pindi mwakani
Kuagana hutokea.

95. Hasa akiwa rafiki
Inazidi hiyo dhiki
Unashindwa kusadiki
Hilo lililotokea.

96. Unashikwa bumbuwazi
Mdomo waacha wazi
Yule mlokibalizi
Idadi imepungua.

97. Rafiki wa itikadi
Huyu rafiki shadidi
Sahibu huyo waridi
Akaapo hunukia.

98. Mkipendana wawili
Kwa ajili ya Jalali
Huo urafiki kweli
Pazuri mwaelekea.

99. Urafiki wa maana
Wa kufa na kuzikana
Hiyo ni kubwa hazina
Ni kazi kuifikia.

100. Urafiki wa imani
Bora hauna kifani
Usuhuba wa thamani
Thamani ilozidia.

101. Thamani kubwa ajabu
Ni urafiki twaibu
Wenye wingi wa thawabu
Wema mnatimizia.

102. Wemamnakumbushana
Mabaya kukatazana
Ili kuipata 'Janna'
Pepo iliyotulia.

103. Kukumbusha kuna cheo
Hususa kwa waaminio
Kukumbusha ufyagio
Takataka kuzitoa.

104. Binadamu ni dhaifu
Tena ana upungufu
Kumkumbusha ni afu
Waweza kumzindua.

105. Huo hasa urafiki
Una faida lukuki
Za kumpata Maliki
Shabaha yetu na nia.

106. Insia pamwe majini
Shabaha yake Manani
Kutuleta duniani
Kuabudu zingatia.

107. Ima alijitahidi
Ibada kwake waridi
Faradhi na tahajudi
Humo aliogelea.

108. Kitabu ili tusali
Katufanyia sahari
Tafsiri kiswahili
Kitabu katutolea.

109. Sala hasa ndio shina
Waislam hakuna
Hadi umeshikamana
Rasuli katuambia.

110. Sala ina taratibu
Kuzifata ni wajibu
Malipo yake thawabu
Rabbi amewawekea.

111. Mtu aso na ibada
Kwetu humuita buda
Hana moja la ziada
Kuweza msaidia.

112. Ja samaki na bahari
Ni hadithi ya Bashiri
Yeye ilimuathiri
Masijidi kazoea.

113. Alipenda Msikiti
Mapenzi yalo ya dhati
Na mwingi wake wakati
Hapa aliutumia.

114. Kuna utamu ajabu
Kwenye nyumba ya Wahabu
Tamu kuliko zabibu
Nyumba iliyotulia.

115. Hino nyumba na Kahari
Masikini na tajiri
Wote waipate heri
Roho zao kutulia.

116. Kukosa Msikitini
Haikuwa asilani
Labda yupo kazini
Nje ya wetu mkoa.

117. Hiyo sifa ya kuiga
Vizuri nasi kujenga
Msikiti unanoga
Moyo hupata tulia.

118. Fungamana na Jamati
Ni ahadi ya baiati
Kutoacha Msikiti
Unaipata jamaa

119. Nayo sala ya jamaa
Fungu lake limejaa
Kuikosa ni balaa
Pasi sababu ajaa.

120. Kaipa kipaumbele
Mbora wa wateule
Katu msiilekele
Ni chakula penye njaa.

121. Sana alijitahidi
Jamaa kupata sudi
Hakukosa wa Saidi
Agizo hilo murua.

122. Akiwa Msikitini
Marafiki wa imani
Wengi aliwathamini
Wengi nakuongezea

123. Si wazee si vijana
Marafikize bayana
Na wote walishibana
Kwa mapenzi ya murua.

124. Akufaaye kwa dhiki
Na huyo ndiye rafiki
Hilo jambo nasadiki
Wengi ametutendea.

125. Matendo yaliyo mema
Yaliyojaa huruma
Kafanya kwa taadhima
Wengi katusaidia.

126. Mkonoe wa kutoa
Ubakhili hakujua
Kwa siri bila kujua
Nini kinachotokea.

127. Atakuita pembeni
Kupapasa mfukoni
Na tabasamu usoni
Alichonacho kutoa.

128. Hata na kazi za ndani
Kwa mfano wa amini
Nguo katia sabuni
Alishiriki kufua.

129. Mfano ulotukuka
Kutenda si kutamka
Na hiyo ndio baraka
Kutega na kutegua.

130. Kusema usiyo tenda
Ni chukizo lina inda
Ni sawa kama kuwinda
Mkuki hujachukua.

131. Hiyo imani dhaifu
Ameibeza Raufu
Vitendo ni ashirafu
Sifa unajichumia.

132. Huo mwendo wake Ali
Alomuhofu Jalili
Na kumtii Rasuli
Yote aloagizia.

133. Kutii na kufuata
Kutenda bila kusita
Mithili yake mafuta
Yanayoiwasha taa.

134. Rafiki mtanashati
Bashasha kila wakati
Ya Rabi Mola idhati
Twaomba kumpokea.

135. Kukunja uso muhali
Alifanya kuli hali
Upate kuwa jamili
Tabasamu kulitoa.

136. Kila mnapokutana
Assalamu atanena
Mikono mtapeana
Pia takukumbatia.

137. Fundisho hilo muhimu
Dini yetu islamu
Sote inatulazimu
Salamu tumezitoa.

138. Salamu siyo hiyari
Bali hiyo ni amuri
Kutoka Mola Kahari
Kuja kwa sisi insia.

139. Sahibu msema kweli
Akimuhofu Jalali
Kwa kutoa yake mali
Wanyonge kusaidia.

140. Hakuwa na ubakhili
Aligawa kwa suruli
Kamjalia Kahari
Kwa mkono wa kutoa.

141. Ajuza huko Kitonga
Karibu tulikojenga
Nyumba hiyo amejenga
Zawadi kumpatia.

142. Kusadi wasojiweza
Mithili huyo ajuza
Wajibu ametimiza
Wanyonge kusaidia.

143. Mtu asiye kinyume
Alisimama kiume
Hata upepo uvume
Katu hakuachilia.

144. Imara kwa itikadi
Ya kufika kwa Mahadi
Seyidina Ahmadi
Mjumbe wake Jalia.

145. Akiwa shule ya Tanga
Ndipo aliona mwanga
Jumuiyyakujiunga
Aloanzisha Masia.

146. Yote akayakubali
Kuendelea Rasuli
Na Isa jambo la kweli
Ametawafu India.

147. Amezikwa Kashmiri
Kwenye vilima vizuri
Lilipo lake kaburi
Wageni pawavutia.

148. Tumwawotewamepita
Kwenda bila ya kusita
Ni amri ya kumeta
Kitabu chake Jalia.

149. KamakafaMuhammadi
Nani akwepe ahadi?
Eleza kwa ushahidi
Nasi tuweze bukua.

150. Hoja ikamuingia
Yote akazingatia
Kweli katika dunia
Issa hawezi tokea.

151. Ukweli wake Mahadi
Seyidina Ahmadi
Kapima bila idadi
Hoja zilizotulia.

152. Mtu akijitangaza
Kwamba Mola kanifunza
Na kunipa muangaza
Wote kuwaangazia.

153. Kama kasema uongo
Mshipa wa kwenye shingo
Atauponda kwa gongo
Bila huruma kutia.

154. Miaka ishirini na tatu
Huwezi kupita katu
Atamezwa nae chatu
Aibu kwenye mitaa

155. Huwezi kuneemeka
Itakufika shabuka
Lazima kuporomoka
Nyumba kujiangukia.

156. Tazama na zingatia
Ahmadiya Jamia
Kote imesha enea
Pembe zote za dunia.

157. Imevunja misalaba
Na nguruwe kuikaba
Ni kazi ya Masahaba
Wale walompokea.

158. Shutuma amezijibu
Kumhusu mahabubu
Sasa wanayo adabu
Hoja zao zimenywea

159. Wamefuata viongozi
Ni viongozi azizi
Tena wanao ujuzi
Kuziongoza mashua.

160. NiKhalifawaMwenyezi
Waletao mbawazi
Wang'arao kama mwezi
Elimu kutupatia.

161. Hizo dalili zatosha
Sisi kutufahamisha
Kwani amekamilisha
Ushahidi ametoa.

162. Imani yake kuzidi
Sababu yake juhudi
Kwa vitabu alizidi
Mapenzi yalokolea.

163. Nacho k itabu kwa siku
Alisoma kwa shauku
Akamtoa mkuku
Adui wa kuto jua.

164. Kavisoma kwa makini
Na kuweka akilini
Alopata vitabuni
Yote akazingatia.

165. Uchoyo hakuwa nao
Nasi kafanya mgao
Tukapanga angalao
Kile alotupatia.

166. Na kavisoma vitabu
Vya Jamaat mahabubu
Huo ni wetu wajibu
Imani kuongezea.

167. Imani yaongezeka
Vitabu vikisomeka
Mengi yaliyofichika
Kuweza kuyatambua.

168. Bila vitabu hatari
Huwezi pata habari
Alozileta Bashiri
Ili kuishika ndia.

169. Sasa tunayo sababu
Ya kuvisoma vitabu
Kwa lugha yetu adhimu
Kiswahili asilia.

170. Udhuru sasa hakuna
Mambo yote nibayana
Katika lugha mwanana
Lugha iliyotulea.

171. Kisha alienda mbio
Kufasiri kwa Kiyao
Wa Bara na wa Mwambao
Waweze kujisomea.

172. Vitabu vyake Masihi
Viwili kwa usahihi
Kafasiri na kuwahi
Nakala hizo kutoa.

173. Hiyo ni kazi adhimu
Alofanya muadhamu
Ya kusambaza elimu
Wayao kufurahia.

174. Vitabu vyake Masihi
Kuvisoma kwetu sudi
Vina elimu zaidi
Rabbi kamfunulia.

175. Ni matone ya asali
Yenye elimu ya kweli
Tena tiba kweli kweli
Maradhi kuyaondoa.

176. Alikuja gawa mali
Masihi wake Jalali
Maana hiyo fasili
Ni elimu zingatia.

177. Usifikiri ni noti
Kugawa kwa kila nti
Mali kutoa ghalati
Ni giza kuliondoa.

178. Kila kitabu wa kwetu
Usipokisoma katu
Angalau mara tatu
Kiburi kimekujaa.

179. Mara tatu kwa akali
Kwako isiwe muhali
Fanya hilo kuli hali
Thawabu kujipatia.

180. Amesema ni kiburi
Tena ni kubwa hatari
Ukikosa uhodari
Mara tatu kupitia.

181. Kumaizi uhodari
Wa ile yake fasiri
Ikawa sasa dhahiri
Aweza piga hatua.

182. Maandiko ya Masihi
Kafasiri kwa shabihi
Uzuri na usahihi
Sifa akajichumia.

183. Kwa agizo la Khalifa
Kapewa kazi ya sifa
Atafasiri kwa afa
Kiyao anachojua.

184. Amri ilipotoka
Tafsiri kwa haraka
Upesi yahitajika
Makao ya Jumuia

185. Akaanza kwa haraka
Na kwa kalamu kushika
Agizo kuliitika
Baraka kujichumia.

186. Kazi ikapambamoto
Kazi hiyo ilo nzito
Yale maneno mazito
Rabbi Alotuletea.

Itaendelea toleo Lijalo

Bw. Mahmood Hamsin Mubiru anawatangazia ndugu wote kwamba yumo katika kuandika historia ya mzee Ali Saidi Mosse ambayo itachapishwa kwa sura ya Kitabu.
Hivyo anamuomba mwanajamaat yeyote mwenye taarifa makhsusi au jambo lenye kusisimua kuhusu mzee Ali Saidi Mosse ambazo angependa ziingie kwenye historia afanye haraka kumtumia taarifa hizo.
Bw. Mubiru anaweza kupatikana kwa simu Na. 0719382930

Mapinduzi ya Kujitolea Mali katika njia ya Allah yaliyoletwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Makala iliyotolewa kwenye Jalsa Salana 2017 na:

Abdulrahman M. Ame sahib

Wakati Allah anapoamua kuwaneemesha watu au umma kwa baraka zake na fadhili zake basi huwataka wajitolee katika njia Yake. Kwa maana nyingine kujitolea katika njia ya Allah ni sharti la lazima ili mtu binafsi na umma kwa ujumla kupata ukaribu na radhi za Allah, kama aya nilizozisoma hivi punde zinavyotueleza.

Kujitolea katika njia ya Allah kunaweza kuchukua sura tofauti sawa na mazingira, lakini kwa ujumla ili kupata radhi na ukaribu wa Allah mtu anatakiwa awe tayari kujitolea kila chake: muda wake, elimu na ujuzi wake, nguvu zake na vipajii vyake vingine vyote, mali yake na heshima yake, na ikibidi hata uhai wake.

Kila Nabii wa Allah aliyekuja alisisitiza kujitolea huku katika njia ya Allah, na kwa hakika hii ni moja ya dalili ya ukweli wa Manabii kwamba: Ni kwa kiasi gani waliweza kuleta mapinduzi ya kujitolea katika njia ya Allah ndani ya maisha yao na ya wafuasi wao.

Hivyo mada iliyopo mbele yetu inakusudiwa kutoa mwanga juu ya jambo hili kwamba mafundisho ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. yameleta mapinduzi au athari gani kwa wafuasi wake katika kujitolea kwao mali katika njia ya Allah, ili apime mwenye kupima na atafakari mwenye kutafakari iwapo mapinduzi hayo yanawezekana kuletwa kwa mipango ya kibinadamu tu yasiyoambatana na matakwa ya kimbingu.

Ikumbukwe kwamba ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ulitabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w kuwa utakuwa ni ufufuo wa Islam baada kuachwa kwake na kutupwa kama falsafa isiyo na maana. Ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ulitakiwa ulete mabadiliko katika kila nyanja ya maisha ya wafuasi wake sawa na mafundisho ya Islam.

Kujitolea mali katika njia ya Allah ni moja ya fundisho la msingi sana katika Islam; bali kujitolea mali katika njia ya Allah hakuwezekani iwapo mtu hajapata imani ya kweli ya uwepo na Utukufu wa Allah. Huu ni ukweli wa kimaumbile kwani mwanadamu ameumbwa na uasili wa kupenda mno mali, na hivyo mpaka pale atakapopata jambo lenye thamani zaidi, lenye kupendeza zaidi na lenye mvuto mkubwa zaidi ya mali ya kidunia katu hakuna nguvu ya kumuondoa kiumbe huyu kwenye huba na mapenzi ya mali.

Na huu nao ni ukweli wa kiroho kwamba iwapo mtu hajang'oa gugu la mapenzi ya mali moyoni mwake, kamwe mti upendezao wa Mapenzi ya Mungu hauwezi kupata nafasi ya kumea kwenye moyo huo huo mmoja; na hii ndio sababu na hekima kubwa ya Mwenyezi Mungu kuweka amri ya kutoa mali katika njia yake kwa kila yule anayetaka radhi na ukaribu wake ili kwamba ile sifa ya kinyama ya kupenda vionekanavyo aweze kuing'oa na mahala pake apandikize mti wa mapenzi ya Yule asiyeonekana, kama asemwavyo Mwenyewe katika Hadithi Qudsi *"Ewe mwanadamu mali ni mali yangu na pepo ni pepo yangu, basi inunue pepo yangu kwa mali yangu."*

Ndugu wasikilizaji, kabla ya kuangalia mapinduzi aliyoyaleta Masihi Aliyeahidiwa a.s. hebu tutupie macho kidogo kwenye kurasa zilizotukuka za maisha ya Mtukufu Mtume s.a.w, ili tuweze kupata pa kupimia.

Mtukufu Mtume s.a.w. yeye mwenye alikuwa wa mwanzo katika kuonesha mfano uliotukuka mno wa kujitolea katika njia ya Allah na hivyo akazalisha mapinduzi hayo ndani ya wafuasi wake kwa kiwango cha kuishangaza dunia.

Mtukufu Mtume s.a.w alipomuoa bibi Khadija r.a., alikabidhiwa mali zote na mke wake huyo wakiwemo watumwa pia; Lakini haukupita muda Mtukufu Mtume s.a.w alishaigawa mali hiyo yote katika njia ya Allah, yaani katika kuwasaidia maskini na wenye shida huku akiwaacha watumwa wote huru na mali nyingine akiitumia katika kuwasaidia watumwa wa watu wengine wengine kununua uhuru wao.

Maisha yote ya Mtukufu Mtume s.a.w yalijaa mifano ya kujitolea mali katika njia ya Allah kwa namna inayoonesha kwamba kitu kinachoitwa mali alikiona kama kizuizi kikubwa baina yake na Mola Wake. Imesimuliwa kwamba wakati fulani Mtukufu Mtume s.a.w aliwahi kupata Dirham 70,000 au 90,000 na hiki kilikuwa ni kiwango kikubwa kabisa cha fedha ambacho Mtukufu Mtume s.a.w aliwahi kukipata katika uhai wake. Lakini mara tu alipopata kiwango hicho hakwenda nyumbani kwake bali alitandika jamvi msikitini na kumwaga kichele hicho chote na kaunza kumpatia kila aliyekuja sawa na shida yake hadi fedha hizo zilipomalizika ndipo akainuka na kuelekea nyumbani kwake.

Mtu anaweza kusema kwamba Mtukufu Mtume s.a.w aliamua kuzigawa fedha hizi kwa sababu zilikuwa nyingi mno na wakati mwingine hutokezea baadhi ya watu wapatapo fedha nyingi za ghafla hupatwa kiwewe cha ulimbukeni na wakadhani kwamba hazitoisha, ingawaje watu wa aina hiyo mara nyingi hufanya isirafu ya kutumia ovyo. Lakini hali haikuwa hivyo kwa Mtukufu Mtume s.a.w kwani hata alipokuwa na dinari chache tu alikimbilia kuzitoa hizo katika njia ya Allah. Akiwa kwenye kitanda cha mauti (yaani ugonjwa wake wa mwisho kabla ya kuondoka duniani) Mtukufu Mtume s.a.w aliwahi kumpatia mke wake bibi Aisha r.a. kiasi cha dinari 7 ili azihifadhi. Alipokumbuka Mtukufu Mtume s.a.w akamuuliza iwapo bado anazo Dinari hizo 7. Bibi Aisha r.a. alipojibu kwamba bado anazo Mtukufu Mtume s.a.w akamuagiza azitoe katika njia ya Allah haraka sana. Baada ya kutoa agizo hilo Mtukufu Mtume s.a.w akaelekea kuzimia na bibi Aisha r.a. akashughulika katika kuangalia hali yake kiasi kwamba akajisahu kuzitoa dinari zile. Baade kidogo Mtukufu Mtume s.a.w akazinduka na swali la kwanza alilomuuliza bibi Aisha ni iwapo alishazitoa fedha hizo. Alipojibiwa kwamba bado, akaziomba apewe na alipopewa akazihesabu na hapo hapo akazitoa katika njia ya Allah kwa mkono wake uliobarikiwa huku akisema Muhammad atamkabilije Mola wake wakati amepewa amana ya Dinari 7 na akashindwa kuzitimizia haki yake ya kuzitoa hadi akafariki bado anazo mikononi mwake?

Huu ndio moyo wa kujitolea wa Mtukufu Mtume s.a.w. ambao uliwabadilisha mno Masahaba zake kaisi hiki kwamba nao walijitolea kila chao katika njia ya Allah.

Mfano wa Hadhrat Abu Talha (ra) aliyejitolea bustani yake iliyo bora na nzuri kabisa katika mji wa Madina ambayo ilikuwa mbele ya msikiti wa Mtume s.a.w.; Mfano wa Abūl Da'daa' (ra) aliyetoa moja ya shamba lake kubwa na bora kabisa huku akiwaondoa mke wake na watoto wake waliokuwemo bustanini humo wakati huo, akiwaambia Allah atakupatieni bustani iliyo bora zaidi ya hii katika maisha yajayo. Mfano wa Hadhrat Abubakar aliyewahi kutoa mali yake yote aliyokuwa nayo wakati huo, itabaki kuandikwa kwa wino wa dhahabu katika historia ya kujitolea katika njia ya Allah. Hii ni mifano mikubwa michache tu lakini kwa hakika Masahaba wote wa Mtukufu Mtume s.a.w walipitana kwa namna moja au nyingine katika kutoa mali zao katika njia ya Allah. Hakuna aliyekubali kubaki nyuma, matajiri kwa maskini, wakubwa kwa wadogo, wanawake kwa wanaume, wote hao, hata kama mmoja wao alikuwa na uwezo wa kutoa kokwa moja tu ya tende, hakujidhani kwamba yeye hana cha kutoa katika njia Allah.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., ambaye ametimiza bishara za ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa na pia bishara za Imam Mahdi akiwa ni mtu mmoja mwenye lakabu mbili, kwa upande wake aliihuisha suna hii ya Mpendwa wake na Kiongozi wake Mtukufu Mtume s.a.w. Suna ambayo kimsingi ilishapotea miongoni mwa Waislam na kila mtu alishazama kwenye kujipatia raha na starehe za dunia binafsi kama mwenyewe Seyyidna *Ahmad a.s. alivyoiweka:*

Wako wapi waumini, waje kuihami dini, wote wamo furahani, na wanawake nyumbani.

Wako wapi Maulama, na wenye fikira pana, dini habari hawana, yashambuliwa na nini.

Dunia wameipenda, hata hadi ya kupenda, mali zao waziponda, kwa furaha za nyumbani.

Ndugu wasikilizaji, nataraji kwamba wengi wetu kama sio wote hapa, tunakumbuka kuwa katika kuufikisha ujumbe wa Allah, mwanzoni tu Masihi Aliyeahidiwa a.s. alijikita kwenye uandishi wa vitabu vya kuutetea Uislamu pamoja na kujibu shutuma za wapinzani, vitabu ambavyo kimsingi ilimbidi kuvigharamia yeye mwenyewe huku akiweka dau la Rupia elfu kumi kwa mtu yeyote atakayeweza kujibu au kuonyesha uzuri wa dini yake yoyote iliyo dhidi ya Islam kwa hata robo tu ya hoja alizozieleza yeye na pia akiahidi kuuza kila chake katika kutimiza ahadi hiyo ya kuutetea Uislamu.

Kwa upande mwingine aliagizwa na Allah kwamba asichoke kuwapokea na kuwahudumia wageni ambao watamfikia mjini Qadian kutoka maeneo mbalimbali kwa lengo la kuushuhudia ukweli wake. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alizibeba gharama za ugeni huo yeye mwenyewe na kila alichopata au alichokuwa nacho alikitumia katika njia ya Allah kana kwamba ni shughuli yake binafsi.

Inakisiwa kuwa kwa muda wa miaka 7 baada ya agizo hili Masihi Aliyeahidiwa a.s. alitembelewa na wageni wasiopungua 60,000. Huu ni wastani wa wageni 23 kwa siku. Alianzisha jiko la umma (Langar Khana) kwa ajili ya wageni na hata wenyeji pia na gharama hizo kimsingi zilikuwa mabegani mwake muda wote, hata kama hiyo ilimaanisha kujinyima yeye mwenyewe na ahali zake.

Mnamo mwaka 1891 Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipoanzisha Jalsa salana sawa na amri ya Allah wageni wengi walimfikia kwa wakati mmoja. Ingawaje walikuwa kama watu 70 tu hivi, lakini watu 70 kwa mazingira ya kijijini, tena ya wakati huo walikuwa ni wengi na kimsingi gharama zote za Jalsa Masihi Aliyeahidiwa a.s. alizibeba yeye mwenyewe kutoka mfukoni mwake kwani ingawaje baadhi ya masahaba zake r.a. walishaanza kujitolea kwa mapenzi ya imani yao lakini utaratibu wa mchango wa Jalsa ambao tunao sasa ulikuwa haujawekwa.

Kwenye Jalsa salana hiyo ya kwanza, inasimuliwa kwamba katika siku ya pili ya Jalsa Hadhrat Mir Nasir Nawab sahib ambaye alikuwa msimamizi upade wa dhiafat alimwendea Masihi Aliyeahidiwa a.s. na kumwambia kwamba chakula kilikuwa kimeisha na hivyo usiku huo wageni wasingekuwa na kitu cha kula. Masihi Aliyeahidiwa a.s. hakuwa na kitu mfukoni mwake na hivyo akamwambia aende kwa *Begum Sahiba* (Mke wake) na kumuomba iwapo ana mapambo yoyote ayatoe ili ipatikane fedha ya kununua chakula. Mama huyo wa waaminio bila kusita alitoa mapambo yake hapo hapo na Hadhrat Mir Nasir akayauza au akayaweka rehani ili kuweza kupata fedha za kununulia chakula cha kuwahudumia wageni.

Mifano hii ni kama tone kwenye bahari ya kujitolea mali katika njia ya Allah ambako Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikufanya, na ni kwa kuathiriwa na sifa hii ya mwalimu wao bora, wafuasi wake nao walikwea vilele vya mifano ya kujitolea ambavyo ukiondoa Maswahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w huwezi kupata mfano wao katika historia ya umma wa kiislam.

Kujitolea kwa maswahaba wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. nako ni kama bahari pana isiyo na ufukwe, kwa kadri mzamiaji au muogeleaji atakavyopiga mbizi atajikutia anaibukia baharini tu na kamwe hawezi kuizunguka bahari yote.

Hapa chini nitaeleza mifano michache tu ya kujitolea mali katika njia ya Allah ambako kumefanywa na wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kuanzia enzi za uhai wake hadi leo ikionesha ni mapinduzi ya kiasi gani yametokea kwa wafuasi wake katika uwanja huu.

Itaendelea toleo Lijalo. Inshallah

-

HUZUR AWAKUMBUKA WATU WENYE MATATIZO YA MACHO BARANI AFRIKA

- ***Azindua Kliniki Inayotembea Kwa Ajili ya Kuhudumia Wagonjwa wa Macho Bure.***
- ***Ni Miongoni Mwa Miradi ya Humanity First Itakayokuwa Ikitoa Matibabu Ikiwemo, Uchunguzi na Operesheni Bure.***

Na: Ayoub SADI - Masjid SALAAM, Dar Es Salaam

Bara la Afrika ni moja ya Mabara yenye kuvutia kutokana na kuwepo kwa utajiri mkubwa wa rasilimali watu na maliasili, ambavyo kwa pamoja vinalifanya bara hili liwe na sifa ya kipekee katika nyanya ya utalii na ubinadamu. Licha ya kuwepo kwa vivutio na wingi wa rasilimali watu katika bara la Afrika, maisha ya binadamu katika bara hili yamekuwa na changamoto nyingi zinazosababishwa na kuibuka kwa magonjwa mbalimbali ukiwemo ugonjwa wa macho ambao husababisha ulemavu wa macho hasa kwa vijana kuanzia umri wa miaka 15-35 na watu wazima wenye umri wa miaka 40-50 waishio katika bara hili.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na shirika la afya duniani ya mwaka 2010, WHO, inakadiriwa kuwa watu wapatao milioni 285 wana matatizo ya macho duniani kote huku watu milioni 39 kati ya hao hawaoni kabisa (vipofu) na wengine 246 milioni wakiwa na uoni hafifu wa macho. Hiyo Ripoti hiyo pia inatanabaisha kuwa asilimia 65 ya watu wenye matatizo ya uoni hafifu na asilimia 82 ya watu wasioona ni wazee wenye umri kuanzia miaka 50.

juu ya hali hiyo *'Polepole Ndio Mwendo'* na *'Haraka Haraka Haina Baraka'* . Ingawa uhalisia wa dunia ya leo, hatua za haraka katika maendeleo ndio jambo linalotakikana sana kuweza kuondokana na changamoto zizolikabili bara la Afrika.

Changamoto ya magonjwa katika bara hili, zimekuwa zikichangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa lindi la umasikini kutokana na kuathiri wengi wa wakazi wa bara hili ambao ndio nguvu kazi inayotegemewa kuzalisha na kuchangia kukua kwa uchumi wa bara hili ambalo sehemu yake kubwa ilipata kutawaliwa na Wazungu kutoka bara la Ulaya wakati wa ukoloni karne moja iliyopita.

Katika kuchangia kupunguza changamoto ya magonjwa iliyopo katika bara hili na kuleta mwanga mpya wa matumaini kwa watu wenye matatizo ya macho, Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Dunia, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a amezindua mpango mpya wa utoaji wa huduma inayotembea ya Macho ikiwa ni mahususi kwa ajili ya watu wa bara la Afrika.

Mpango huo mpya kabisa



Pichani: Muonekano wa nje wa Kliniki Inayotembea ya Al Ain. (Picha na Ayoub Sadi kwa msaada wa Maktaba ya Makhzan Tasaweer).



Pichani: Muonekano wa sehemu ya ndani ya chumba cha uchunguzi wa macho katika kliniki ya Al Ain iliyozinduliwa na Khalifatul Masihi V a.t.b.a nchini Ujerumani tarehe 23 Aprill 2017. (Picha na Ayoub Sadi kwa msaada wa maktaba ya picha za Jamaat mtandaoni, Makhzan Tasaweer.

Licha ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na mashirika ya huduma za kibinadamu ulimwenguni, lakini bado bara hili limekuwa likikubwa na vikwazo ambavyo kwa namna moja ama nyingine vinalifanya bara hili lishindwe kupiga hatua za haraka katika kuyaendea maendeleo endelevu japo kuna methali za wahenga zinazotumiwa sana na waswahili kujipa moyo

unaoitwa ***Al Ain,*** maneno ya kiarabu yenye maana ya **JICHO** umezinduliwa rasmi na Huzur katika mji wa Frankfuirt nchini Ujerumani tarehe 23 Mwaka huu ikiwa ni sehemu ya Mradi wa shirika la Jamaat la Humanity First chini ya Progaramu maalumu iitwayo ***Zawadi ya Macho (Gift of Sight).***

Kliniki hiyo inayotembea katika gari maalumu lenye kubeba trela kwa nyuma , itakuwa ikitoa matibabu ya bure ikiwemo kufanya upasuaji wa mtoto wa jicho (Cataract), huduma ya macho, uchunguzi na ushauri wa kitaalamu kwa watu wenye matatizo ya macho katika bara la Afrika, hasa wale waliopo katika maeneo ya vijijini.

Uzinduzi wa mradi huo ulifanyika katika msikiti wa Baitus Sabuh; moja ya misikiti mipya uliofunguliwa na Huzur wakati wa ziara yake aliyoifanya nchini Ujerumani mapema mwezi huu.

Kwa kuzindua mradi huo mpya, Huzur amewahakikishia mamilioni ya Waafrika hasa wanajamaat wenye matatizo ya macho ambao hawakuwa na uwezo wa kumudu gharama za matibabu, uhakika wa usalama wa macho yao pasipo wao kuchangia kiasi chochote cha pesa. Kwa maana nyingine, Mradi wa Al Ain, umekuja kuwa suluhisho la magonjwa ya macho kwa watu masikini waishio katika maeneo mbalimbali ya bara la Afrika.

Mpango wa Al Ain miongoni mwa miradi inayofadhiliwa na shirika la Humanity First ambalo limejikita zaidi katika kuwahudumia viumbe wa Allah kwa kutoa misaada mbalimbali ya kibinadamu katika nchi zilizokumbwa na maafa, kujenga shule pamoja na huduma ya umeme

Wakati akihudumia mkutano ulioandaliwa na shirikala la Humanity First, Januari mwaka 2015, Huzur alisema:

"Kuhudumia binadamu kunahitaji mtu asipumzike mpaka kwanza ahakikishe ametatua matatizo yaw engine na kuzibeba shida za wengine katika mabega yake. Inahitaji moyo wa mtu uwe na mapenzi kwa wengine ambapo mtu huyo hujali zaidi furaha na raha za wengine. Inahitaji mtu awe tayari kukumbana na kilaaina ya shida kwa ajili yaw engine na kuyachukulia maumivu yaw engine kama maumivu yake mwenyewe. Inahita mtu awe tayari kubeba mahangaiko binafsi au hofu yake ili kwamba wengine waishi katika hali ya amani na kutosheka"



Khalifatul Masihi V, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a akiongoza dua ya kimya kimya baaday a kuzindua mradi wa Huduma Itembeayo ya Macho uitwao Al Ain, mjini Frankfuirt, Ujerumani tarehe 23 Aprill 2017. (Picha na Ayoub Sadi kwa msaada wa maktaba ya picha za Jamaat mtandaoni, Makhzan Tasaweer).

Ziara za Amir mikoani zaleta neema



Kulia: Amir sahib akifungua madarasa mapya manne ya Jamia Ahmadiyya. Kushoto: Amir sahib akiongoza maombi ya kimya baada ya uwekaji wa jiwe la msingi la madarasa ya shule za awali na msingi za Ahmadiyya.

Kutoka uk. 12

kumjua Mwenyezi Mungu. Endapo jamii itakuwa na hofu ya Mungu itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza au hata kumaliza kabisa vitendo viovu katka jamii ikiwemo mauaji ya watu ambao wasio na hatia kama vile vikongwe na watu wenye ualbino" Amir sahib alitoa utangulizi wa Jumuiya kwa mgeni rasmi na kumfahamisha ya kwamba Jumuiya ina miaka 6 mkoani hapo ikisambaza mafundisho ya amani na kutenda wema na kufanikiwa kujenga misikiti 20 pamoja na ile ya Simiyu. Pia Jumuiya imekuwa mstari wa mbele katika kutoa huduma ya maji kwa watu bila kuangalia dini wala kabila na kuweka umeme wa nishati ya jua katika misikiti yetu ambayo pia husaidia jamii inayozunguka.

Mkuu wa mkoa wa Shinyanga alipatiwa nafasi ya kutoa nasaha na Amir sahib na aliomba viongozi wa dini mbalimbali kuhamasisha amani katika jamii na kutoa mafunzo kwa waumini wao. Aidha aliipongeza Jumuiya kwa jitihada inazozifanya katika kuhubiri amani katika jamii na kukemea vitendo viovu ikiwemo mauaji ya wasio na hatia ikiwemo vikongwe na watu wenye ualbino pamoja na kuwanyanyasa wanawake na watoto katika jamii pia aliiomba Jumuiya iendelee kufanya mikutano ya namna hiyo mara kwa mara ili jamii ielimike na kuendeleza mchango wa maendeleo ya jamii. Mwisho alishukuru kwa kufanywa kuwa mgeni rasmi katika mkutano huo na kuahidi kuendeleza ushirikiano na Jumuiya katika kulijenga taifa.

Jalsa ilihutubiwa na masheikh toka mikoa mbalimbali na walimu pia. Hotuba hizo zilihadhiri kwa majina; "Umuhimu wa Wanawake na Watoto katika Jamii na Ndoa", "Nafasi na Umuhimu wa Sala", "Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ndio inawakilisha Uislam wa Kweli" na "Baraka za Ukhalifa"

Mwisho Amir sahib aliwashukuru wahudhuriaji wapatao 1600 kwa kufika na kuwaombea kwa Allah Awape baraka zipatikanazo katika kushiriki kwenye Jalsa Salana na akawaasa kuwa ni lazima tuhakikishe tunajifunza na kuwafundisha watoto wetu juu ya Jumuiya Ahmadiyya.

Tarehe 10/07/2017 ulifunguliwa msikiti kata ya Imesela, Shinyanga Vijijini uliotumia takribani miezi mitatu ya ujenzi.

Wanajamaat waliohudhuria ufunguzi waliusiwa kushikamana na Jamaat ili wapate baraka na kuitafuta elimu ya dini kiukamilifu. Pia Amir sahib aliwaasa wanajamaat kuuhifadhi msikiti huo kwani ni kituo kizuri cha kukutana na kumuabudu Mwenyezi Mungu.

Diwani wa kata aliishukuru Jumuiya kujenga msikiti mzuri namna ile ambao haukuwahi kufikiriwa kujengwa katika kijiji hicho na kuleta mabadiliko makubwa na muonekano wa kata yake na akashauri kujengwa kwa shule kama itawezekana.

Mnamo 11/07/2017 ilifunguliwa misikiti miwili iliyopo Butibu na Kasomera wilayani Ushetu na nyumba ya mwalimu.

Mnamo 12/07/2017 ulifunguliwa msikiti kata ya Samuye, Sakabai wilaya ya Shinyanga Vijijni

ZIARA SIMIYU

Amir Jamaat akiambatana na Sheikh wa kanda ya ziwa na baadhi ya wajumbe wa Majlis Amila Taifa alizuru tawi la Mitobo mnamo 13/07/2017. Ni tawi jipya lililomlaki vizuri sana. Amir sahib aliwaeleza wanatawi katika kikao nao ya kwamba wamefanya maamuzi sahihi ya kumpokea Masihi Aliyeahidiwa kwani ndiye aliyetumwa na Allah katika zama hizi kwa niaba ya Mtume Muhammad (s.a.w). Hivyo Amir sahib aliwataka wanajamaat hao kujitambua ya kwamba maadamu wamejiunga na Jumuiya hii basi wawe ni watu wema na wajiepushe na kila jambo ovu.

Amir Jamaat na ujumbe wake walimtembelea Mkuu wa Mkoa wa Simiyu ndugu Antoni Mtaka ofisini kwake tarehe 14/07/2017 . Amir sahib alimpatia maelezo kuhusu Jamaat Ahmadiyya na alimuelezea shughuli zinazoendelea sasa za ujenzi wa misikiti mitano pamoja na nyumba za waalimu sambamba na huduma za kijamii zilizofanyika za uchimbaji visima 5 vya maji katika makazi ya watu. Mkuu wa mkoa alipongeza juhudi hizo na kuomba kuandikiwa ombi la eneo kwa ajili ya kufungua makao ya mkoa kwa kujengea msikiti na huduma nyingine mbalimbali.

Ijumaa hii hii ilifanyika Jalsa Salana ya kwanza mkoani Simiyu katika Jamaat ya Migato umbali wa kilometa 60 kutoka Simiyu. Katika hotuba ya ufunguzi wa Jalsa hiyo Amir sahib aliwaasa wanajamaat akisema "Jalsa ni mkutano ambao ulianzishwa na Masihi aliyeahidiwa a.s. na hivyo ni mkutano wenye baraka kubwa" na aliwaomba waliohudhuria kuwa wasikivu ili wapate faida ya mkutano huu. Hotuba ya kwanza ilitolewa na Rais wa kanda ya ziwa, Mzee Salum Thani iliyohusu "*Imani Juu Ya Mungu*", kisha Sheikh wa kanda hiyo, Sheikh Waseem Ahmad Khan akatoa hotuba ya "Nguzo za Islam". Hotuba ya mwisho iliyokuwa na anuani *"Utambulisho Wa Jumuiya Ya Waislamu Waahmadiyya"* iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Ziada, Sheikh Abdulrahman M. Ame. Mwishoni Amir sahib aliwashukuru wahudhuriaji wa Jalsa hiyo takriban elfu moja (1000) kutoka Jamaat kumi za mkoa wa Simiyu yaani Bariadi, Itimila, Budala Bujiga, Mitobo, Kisesa, Madilana, Mhunza, nangale, Ikindilo na Migato na kuwasihi wajitambue na wafuate nidhamu za Kijamaat na wawe tayari kujitolea kwani ndio watakuwa wakitekeleza wajibu wa kujiunga na Jamaat.

Baada ya kuongoza maombi ya kufunga Jalsa Salana, Amir sahib alifungua nyumba ya mwalimu katika Jamaat ya Migato.

Jumamosi ya Julai 15 ulifunguliwa msikiti pamoja na nyumba ya mwalimu katika Jamaat ya Mhunze. Akitoa hotuba ya ufunguzi, Amir sahib alisema kwamba msikiti ni nyumba za Allah hivyo akawataka wakazi wa kijiji hicho kuingia msikitini kwani hiyo ndiyo nyumba ya amani. Pia aliwataka wanajamaat kutambua wajibu wao kwa msikiti kwa kuingia na kusali na kuusafisha.

Ufunguzi mwingine wa msikiti na nyumba ya mwalimu ulifanyika katika Jamaat ya Itilima Jumapili ya tarehe 16 Julai. Katibu Tawala wa Wilaya alihudhuria ufunguzi huo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Itilima na alisema kuwa amefurahishwa sana kualikwa na Waislamu katika hafla hiyo kisha akapongeza hatua hiyo iliyofikiwa na kutoa ahadi ya ushirikiano kati ya ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Jamaat katika masuala mbalimbali. Akitoa hotuba ya ufunguzi, Amir jamaat alisema kwamba msikiti ni nyumba ya Mwenyezi Mungu ambapo Waislamu huingia na kufanya ibada. Pia aliwatanabahisha kwamba wanakaribishwa watu wote waingie katika nyumba hii ili kuja kujifunza tabia njema. "Kila mwanajamaat atambue kuwa kitendo cha kujiunga na Jamaat ina maana amempokea Masihi aliyeahidiwa a.s. hivyo lazima ajue tofauti hii ya msingi" alisema Amir sahib akihitimisha hotuba hiyo ya ufunguzi.

ZIARA MOROGORO

Amir Jamaat Tanzania alizuru mji wa Morogoro Novemba Mosi mwaka huu na kuweka mawe ya msingi ya madarasa mapya na maktaba za shule ya awali ya Ahmadiyya na shule ya msingi ya Ahmadiyya zilizopo Kihonda.

Siku hiyo pia Amir na Mbashiri mkuu alifungua madarasa mapya manne ya Jamia Ahmadiyya. Jiwe la msingi la madarasa hayo yenye miundo mbinu ya kisasa liliwekwa na Mkuu wa chuo - Sheikh Abid Mahmood Bhatt - mwaka 2015 na ujenzi ulikamilika Oktoba mwaka huu.

Jamia Ahmadiyya ni taasisi ya kielimu ilyoanzishwa na Khalifatul Masih wa tatu r.h. kwa lengo la kuandaa wabashiri watakaosambaza dini tukufu ya Islam ulimwenguni. Kwa takriban miaka 33 hapa Tanzania, Jamia Ahmadiyya imepitia duru mbalimbali tangu kuwepo kwake; Masjid Salaam kisha Masjid Nusrat - Morogoro Mjini hadi kuhamishiwa Kihonda kwa muongozo maalum wa Khalifatul Masih wa tano a.t.b.a mwaka 2007. Chuo kimekuwa kikitumia majengo ya iliyokuwa hospitali ya Ahmadiyya yenye umri wa miaka takriban 29 yaliyoonekana kutosheleza hapo kabla. Kuja kwa maendeleo ya siku hadi siku ikiwemo uanzishaji wa darasa maalum la Hifdh Quran kumebainisha haja ya utanuzi.

Katika hotuba yake katika hafla hiyo Amir sahib aliwakumbusha wahudhuriaji juu ya baraka za Allah zimiminikazo katika Jamaat hivyo kuwepo uhitaji wa walimu zaidi. Aliendelea kusema kuwa wengi wanaojiunga hawana elimu ya kidini hivyo huhitaji malezi ya msingi ili kuwaimarisha. Aliwataka wanafunzi wasome kwa bidii na kwa shauku ya kuitumikia dini tukufu ya Islam. Mwisho aliwataka wanachuo pamoja na watumishi kuyatumia vizuri madarasa hayo ili yaweze kutusaidia kwa muda mrefu.

Utii wa kweli kwa Mtume (saw).

Kutoka uk. 12

vikwazo dhidi ya nchi ya Iran, na jambo hili limetokea kinyume kabisa na matarajio ya nchi zote za UIaya, na Umoja wa nchi za Ulaya na nchi nyingine pia wapo kinyume na maamuzi haya. Hata Uingereza, oradha imeandikwa kuwa dunia kwa ujumla ipo kinyume na uamuzi huu wa Rais wa Marekani. Hata hivyo, kuna nchi tatu ambazo wanasema nchi ya Marekani wamefanya uamuzi sahihi.

Marekani yenyewe ni miongoni mwao, na nchi ya pili ni Israeli na Nchi ya tatu ni Saudi Arabia. Kwa sasa, Saudi Arabia wameruhusu nchi ya wasio Waislam kuendeleza vita dhidi ya nchi ya kiislam. Kwa hakika, ni kama wanawaunga mkono. Hivyo, hizi ndio hali za Waislam na hasa hivi ndivyo Masih Aliyeahidiwa (a.s) alivyoonyesha taswira yao alipoeleza kuwa Waislamu watagawanyika. Je ni kwa namna gani watapata Baraka za Allah Mwenyezi?

Masih Aliyeahidiwa (a.s) anasema: "Ninasema kweli kabisa na kwa hakika kulingana na uzoefu wangu kuwa hakuna anayeweza kufanya mambo kwa uadilifu hasa, kupata ukaribu na Allah Mwenyezi, wala kupata faida ya haya, Baraka, hekima za ndani, imani na njozi za kweli, ambazo zinapatikana baada ya kufikia daraja ya juu ya kujisafisha kiroho….. mpaka mtu ajilazimishe mwenyewe kumfuata Mtukufu Mtume (saw)" (wakati mtu anapofikia daraja la juu la usafi wa roho, ni hapo tu ambao atapokea Baraka na kheri kutoka kwa Allah Mwenyezi na kupata njozi na kupata baraka za kuwasiliana na Allah Mwenyezi)". Zaidi ya hilo, ushahidi wa hili unapatikana katika kila neno la Mwenyezi Mungu mtukufu kama alivyosema, "Ikiwa mnampenda Allah, nifuateni, basi Allah atawapendeni".

Masih Aliyeahidiwa (as) anasema: "Mimi mwenyewe ni mfano na uthibitisho wa kweli wa kauli hii. Katika zama hizi, Allah Mwenyezi anawasiliana na mimi baada ya kuzama mimi mwenyewe katika dhati ya mapenzi ya Mtukufu Mtume (saw) na kumfuata kikamilifu. Kufuatia haya, Allah Mwenyezi amenionyesha mapenzi yake pia."

Hivyo, kwa kuwajibu wale wanaoleta upinzani dhidi ya Masih Aliyeahidiwa (a.s) kuwa amefifisha hadhi ya Mtukufu Mtume (saw), Masih Aliyeahidiwa (a.s) amethibitisha yeye mwenyewe kuwa hadhi aliyoipata ni kwa sababu ya mapenzi na kumfuata kikamilifu Mtukufu Mtume (saw). Kuhusiana na kazi aliyopewa kwa sababu ya kujitupa huku kikamilifu kwa Mtukufu Mtume (saw) Masih Aliyeahidiwa (as) anasema: "Nimetumwa tena ili kurudisha ule ukuu wa Mtukufu Mtume (saw) uliopotea na kuidhihirishia dunia ukweli wa Quran tukufu na yote haya yameshaenea. Ingawa, wale wenye mapazia katika macho yao hawawezi kuona haya."

Masihi Aliyeahidiwa (as) anaendelea kwa kusema: "Madai yenu kuwa mna mapenzi kwa Allah Mwenyezi yatathibitishwa kuwa ya kweli na kamili kama tu mtamfuata Mtume Mtukufu (saw)." Anasema "Ni dhahiri kutokana na aya hii kwamba mtu hawezi kuwa mpendwa wa Mungu na mwenye kustahiki ukaribu Naye kwa mtu huyo kujibunia mbinu za vitendo na jitihada za kiroho. Mng'aro wa kimbingu na Baraka haviwezi kumshukia yeyote mpaka mtu huyo awe amejilowesha kabisa katika utii wa Mtume Mtukufu (saw). Mtu aneyejitupa mwenyewe katika mapenzi ya Mtume Mtukufu (saw) na anastahmili kila aina ya mtihani, anapokea mnururisho wa imani ambao unamweka huru na kila kitu isipokuwa Mungu na unamuepusha na madhambi na inakuwa ndio chanzo cha wokovu. Anaishi maisha ya kiucha Mungu katika dunia hii na anaokolewa asidumbukie kwenye kaburi jembamba lenye giza la tamaa za nafsi. Hili limetajwa katika Hadithi moja, ambapo Mtume Mtukufu (saw) alisema: "Mimi ndiye mfufua wafu na watafufuka kupitia kwangu." Wafu wa kiroho wanafufuliwa na Mtume Mtukufu (saw) na wafuasi wake wanakuwa wapendwa wa Allah Mwenyezi. Hivyo, wale ambao kweli ni watiifu wanainua viwango vya matendo yao ya kiibada. Kila mmoja wetu ni lazima alitafakari hili na ni lazima tuboreke kuhusiana na hili vinginevyo madai yetu ya utawa na utii yatakuwa ni unafiki.

Akitoa maoni yake kuhusu imani timilifu ya Mungu aliyokuwa nayo Mtume Mtukufu (saw), Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: "Sema, 'kama unampenda Allah, nifuate: kisha Allah Atakupenda." Mtu anaweza kuwa kipenzi cha Mungu kwa kuwa na utii kamilifu kwa Mtume Mtukufu (saw). Hii inatupelekea sisi kuamini kwamba kwa imani timilifu ya Mungu, yeye alikuwa ni mfano wa kuigwa."

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: "Mtu hawezi kujenga mapenzi kamilifu ya Allah Mwenyezi bila kutumia sifa za kikhulka za Mtume Mtukufu (saw) kama muongozo wake. Hivyo, Allah Mwenyezi Anasema "Sema, kama mnampenda Allah, nifuateni: kisha Allah Atawapendeni." Utii wa kweli kwa Mtume Mtukufu (saw) ni kutwaa khulka zake.

Na kwa hiyo kwanza kuna ufafanuzi kuhusu ibada na pili kuna ufafanuzi kuhusu viwango vya juu vya khulka. Kuwa mfuasi wa kweli kuna maana ya kujiingizia sifa bainifu za kikhulka ambazo zimeelezwa ndani ya Kuruani Tukufu. Kwa hiyo, hii ndio sababu ni kwa nini ni lazima kwetu kuisoma Kuruani Tukufu. Kabla hatujawashauri wengine, tunapaswa kutathmini hali yetu sisi wenyewe kwamba baada ya kumpokea Masihi Aliyeahidiwa (as), ni kwa kiasi gani tumeifanya Kuruani Tukufu kuwa ndio Sheria inayodhibiti matendo yetu na kuiingiza kwenye Baiati yetu? Ni kwa daraja gani tunakuwa imara kuhusiana na ukweli na haki? Ni kwa kiasi gani tunafanya jitihada ya kutetea haki za wengine.

Kisha Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: Njia moja ya kumridhisha Allah Mwenyezi ni kuonyesha utii wa kweli kwa Mtume Mtukufu (saw). Tunaona kwamba watu wanajihusisha katika kila aina ya tamaduni na mila. Bidaa zilizobuniwa sio tu kwamba zinakiuka maagizo ya Mtume Mtukufu (saw), bali kwa namna moja zinakuwa ni tusi kwake. Ni kana kwamba hawamuoni Mtume Mtukufu (saw) yu atosha kwani kama wangefanya hivyo, kwa nini wanahitaji kujidhalilisha chini kiasi hicho kwa kutengeneza hizi tamaduni na mila'

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: 'Hivyo, ni dhahiri kutokana na aya hii kwamba mpaka pale mtu anapomfuata kikamilifu Mtume Mtukufu (saw), hawezi kupata Rehema na Baraka za Allah Mwenyezi na wala hajaaliwi utambuzi na busara ambayo itaepusha dhambi kwenye maisha yake na matamanio ya nafsi yalipukayo. Maneno "Maulamaa wa umati wangu" yanawahusu watu wa aina hii'

Katika sehemu nyingine, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: 'mtu anayesema kwamba uwokovu unaweza kupatikana bila ya Mtume Mtukufu (saw), anadanganya kwani hilo ni kinyume kabisa na kile ambacho Mungu Mwenyezi Ametufundisha. Mungu Mwenyezi Anasema: Kwamba, Ewe Mtume Muhammad (saw)! Waache watu wajue: Kama mnampenda Mungu Mwenyezi basi nifuateni: kisha Allah Atawapendeni. Bila ya kufuata Mtume Mtukufu (saw) hakuna mtu anayeweza kupata wokovu. Wale wanaoweka uadui dhidi ya Mtume Mtukufu (saw) pia watawajibishwa. Hii ni sehmu ya imani yetu.'

Katika tukio moja, Masihi Aliyeahidiwa (as) alikuwa na mdahalo na Mkristo mmoja kwa namna ya kuleta maswali na majibu. Yule Mkristo akatoa nukuu kuhusiana na hadhi ya Yesu (as) ambapo Yesu (as) anasema:

'Njooni kwangu, enyi wenye mahangaiko na mliolemewa na nitawapeni pumziko.' Yesu (as) pia alisema, 'Mimi ni mwanga' na mimi ni njia, ukweli, na uzima. Kwa maneno mengine, alisema kwamba yeye ndio mwanga, anayeonyesha njia na anayetoa uzima, hivyo waende kwake. Kutokana na hilo msomi wa Kikristo akauliza swali kwamba muanzilishi wa Isam, Mtume Mtukufu (saw), aliwahi kujieleza kwa maneno hayo?

Masihi Aliyeahidiwa (as) alijibu hili na akasema: 'Kuruani Tukufu inasema waziwazi: yaani, "Sema, Kama mnampenda Allah, nifuateni: kisha Allah Atawapendeni na Atawasameheni makosa yenu" Masihi Aliyeahidiwa (as) anaendelea kusema: 'Ahadi, kwamba kwa kumfuata Mtume Mtukufu (saw) mtu anapendwa na Mungu, inayashinda yote aliyosema Masiha (as), kwani hakuwezi kuwa na cheo kikubwa zaidi ya kupata upendo wa Mungu. 'Yesu (as) alisema kwamba njooni na mpokee nuru, lakini Mungu Mwenyezi hapa anamwambia Mtume Mtukufu (saw) kwamba atangaze kuwa mtu anayemfuata anaweza kuwa mpendwa wa Mungu Mwenyezi na pia madhambi yake yatasamehewa. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi: 'ni nani mwenye thamani kubwa anayejitangaza kuwa yeye mwenyewe ni nuru au yule anayeongoza kwenye pendo la Mungu?'

Kisha Masihi Aliyeahidiwa (as) akatoa hoja nzuri sana kutoka kwenye aya, "Sema, kama mnampenda Allah, nifuateni…" ili kuthibitisha kwamba Yesu (as) Alishafariki. 'Kifo kimejumuishwa kwenye Sunna ya Mtume Mtukufu (saw) (yaani Mtume Mtukufu (saw) pia alipitia kifo). Mtume Mtukufu (saw) alifariki sasa nani anaweza kupenda kuishi milele au athibitishe kuwa mwingine yoyote anaishi milele..' Upendo wa kweli unahitaji kwamba mtu azame kabisa katika unyenyekevu kwa Mtume Mtukufu (saw) kiasi kwamba awe na udhibiti kamili wa tamaa zake za ndani na atafakari kwamba yuko katika umma gani. Katika hali kama hiyo ambapo mtu anakuwa na imani kwamba Yesu (as) bado yungali hai mbinguni, anawezaje tena kujisema kuwa anampenda na kumfuata Mtume Mtukufu (saw)? Kwa sababu anakubali kwamba Yesu (as) aoenekani mwenye daraja la juu zaidi na anamtaja Mtume Mtukufu (saw) miongoni mwa wafu na anaridhika akiamini Yesu (as) kuwa bado yu hai.

Kwa upande mmoja wanadai kumpenda Mtume Mtukufu (saw) na kufuata amri zake, lakini kwa upande mwingine, kwa kukubali kwamba Masiha (as) yu hai mbinguni wanamkubali yeye kuwa bora zaidi. Hivyo basi, katika siku hii na zama hizi ni Masihi Aliyeahidiwa (as) peke yake ambaye anaitetea Islam na Mtume Mtukufu (saw) dhidi ya kila shambulio, pamoja na kuinua cheo chake. Hili ndilo lililokuwa kusudio la kutokea kwa Masihi Aliyeahidiwa (as), lakini mashekhe wa Kiislam wanabaki wakitoa shutuma dhidi yake.

Masihi Aliyeahidiwa anaendelea kusema: "Ni imani yangu ya dhati kwamba bahati mbaya na majanga yaliyowakuta (yaani Waislam wanaoamini kuwa Yesu (as) yu hai) ni kutokana na ukweli kwamba wamewapa mapadri fursa ya kutosha kumtukana na kumdhalilisha Mtume Mtukufu (saw). Hali ya Waislam inatokana na sababu hii tu. Masihi Aliyeahidiwa (as) anafafanua zaidi: "Kwa upande mmoja wanatamka ki mdomo kwamba Mtume Mtukufu (saw) ni mkubwa kuliko Mitume wote, yaani Mtume Mtukufu (saw) ndiye mwenye cheo cha juu kuliko Mitume wote, wakati kwa upande mwingine wanaamini kwamba alifariki baada ya miaka sitini na tatu na Masihi (as) yu hai mpaka leo hii.. Wana bahati mbaya kiasi gani watu hao hao wanaojinasibisha kwa Mtume Mtukufu (saw), wanamtaja amekufa (Mungu Apishie mbali)"

Baada ya kutaja ukweli kwamba baada ya Mtume Mtukufu (saw) hakuna Mtume aliyepita anayeweza kutokea, yaani kwa kuwa Yesu (as) alikuwa ni Mtume kwa silsila ya Musa (as) na amefariki, kwa hiyo hakuna Mtume wa Silsila ya Musa anayeweza sasa kutokea, kisha Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: "Baraka hii inaweza kupatikana tu kwa utii kamili wa Mtume Mtukufu (saw), kwa sababu ni Mtume Mtukufu (saw) peke yake ambaye ni Mtume hai.

Hivyo, kutokana na utii kamili kwa Mtume Mtukufu (saw), Mungu Mwenyezi Amemtuma Masihi Aliyeahidiwa (as) katika zama hizi akiwa ni Mahdi anayesubiriwa na Masiha. Hadhi yake ni ile ya mtumishi, Mtume asiye na sharia.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: "Mtu anapompenda Mungu Mwenyezi kwa moyo wote kupita vitu vyote vya kidunia, na utukufu na ufalme wa vitu vyote ghairi ya Mungu unaondolewa kwenye moyo wake – kwa hakika anakiona kila kitu kingine kuwa sawa na mdudu aliyekufa – hapo ndipo Mungu Mwenyezi Anamshukia kwenye moyo wake kwa dhihirisho kubwa, kana kwamba kioo safi kinawekwa mbele ya mwezi, kutokana na kuakisi kwa mwezi, inaweza kusemwa kimajazi kwamba mwezi ule ule ulio mbinguni umo kwenye kioo. Kwa mantiki hiyo hiyo Mungu Anashuka kwenye moyo huo na Anaufanya moyo huo kiti Chake cha enzi. Hii ndio sababu kwa nini mtu ameumbwa." Hivyo, Masihi Aliyeahidiwa alikuwa ni mfuasi kamili wa Mtume Mtukufu (saw) na ni kwa sababu hii Mungu Mwenyezi Alimpenda na Akampa heshima kwa kumtaja kuwa Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi na pia kuwa Mtume Mtumishi.

Baada ya kumkubali Masihi Aliyeahidiwa (as), ninamuomba Allah Mwenyezi Atuwezeshe kumthamini na pia Atuwezeshe kuwa wafuasi kamili wa Mtume Mtukufu (saw). Ninamuomba Amuwezeshe kila mmoja wetu kufuata mfano wa Mtume Mtukufu (saw) sawa na uwezo wetu na vikomo, na ninamuomba Awawezeshe Waislamu wamkubali na kumfuata mfuasi makini wa Mtume Mtukufu (saw). Amin.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Rabiul Awwal 1439 AH | NOVEMBA 2017 | Nubuwwat 1396 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Mtu anaifuata dini ya rafiki yake. Hivyo mmoja wenu aangalie anajichagul;ia nani kuwa rafikiye. (*Abu Dawud*).

Utii wa kweli kwa Mtume (saw).

Na Hafidhu Nakuchima

Hadhrat Khalifatul Masih V atba, (Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani) alitoa hotuba katika msikiti wa Baitul Futuh mjini London, ambapo alizungumzia juu ya Utii wa kweli wa Mtume s.a.w.

Baada ya *Tashahhud, Taa'udh* na *Surat Fatihah* Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisema:

Katika hotuba ya Ijumaa iliyopita, nilisoma dondoo ya Masih Aliyeahidiwa (a.s), ambayo alisema ulikuwa ni muda wa Masih kudhihiri ili kuwarekebisha Waislam, kwa sababu ya Waislam kujiweka mbali wao wenyewe na kiini cha Islam, na kwa haki hawana habari ya maana ya kweli na lengo la Islam. "Ni kweli Waislam wanatamka Kalima, wanasimamisha sala, wanafunga katika siku za miezi ya saumu na wanatoa Zakat". Masih Aliyeahidiwa (a.s) anasema, "Nilishasema kwamba matendo yao yote hayana ile maana ya kweli ya ucha Mungu. Vinginevyo ikiwa hivi ni vitendo vya kiucha Mungu, Je ni kwanini havileti matokeo mazuri?" Leo tunaona kuwa machafuko yaliyokithiri yanaonekana katika nchi za Kiislam, tunaona kuwa tamaa ya vitu vya kidunia imeenea kila mahala na watu wanatumia jina la dini kutimiza dhamira zao za kisiasa na kulinda heshima zao.

Ingawaje, maneno yafuatayo yaliyotamkwa na Hadhrat Aisha (ra) kuhusiana na khulka za Mtukufu Mtume (saw) yanafaa kuandikwa kwa wino wa dhahabu. Yaani, "*Kaana Khuluquhu al-Quran* yaani ikiwa mnataka kujua sifa na tabia zake, basi someni Qurani Tukufu, ambayo imeelezea maisha yake na sifa zake kwa kina".

Hivi ndivyo Allah Mtukufu alivyosema kuwa, huwezi kuanzisha uhusiano wa kweli na Mimi kwa kutamka tu *La ilaha illAllah* (Hakuna wa kuabudiwa isipokuwa Allah). Bali, ikiwa mnataka kupata mapenzi yangu, basi mfuateni Mtume Wangu kipenzi na igeni tabia zake, mtafikia katika daraja ile ya kupata ukaribu na Allah. Vinginevyo, maneno yenu yatakuwa ni maneno matupu. Hiyo, Allah Mtukufu anasema, "**Sema: Ikiwa ninyi mwampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni, Mwenyezi Mungu Atawapendeni na Atawaghofirieni madhambi yenu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye ghofira, Mwenye rehema**". (Sura 3:32)

Je hali ya Waislam leo hii inaweza kuwa ya wale wanaopendwa na Allah Mtukufu? Wanazuoni ndio ambao wanasababisha machafuko katika dunia. Wamesababisha kwa ujumla hali ya hofu, ugaidi, machafuko na uharibifu kwa kuruhusu sheria zinazoenda kinyume na yule aliyekuja kutoka kwa Allah Mwenyezi. Kila siku kuna shutuma zinazoongezeka dhidi ya Masih Aliyeahidiwa (a.s) kuwa, Allah Aepushie mbali, ameanzisha Jamaat ili atimize na apate matakwa yake ya kidunia na pia akuze hadhi yake. Hata hivyo, tunafahamu kuwa yeye alikuwa mtumishi mwenye jazba wa Mtukufu Mtume (s.a.w) na Allah Mwenyezi Alimtuma ili akamilishe usambazaji Sheria ya Mtukufu Mtume (saw).

Ili kufafanua zaidi juu ya aya hii, inayosema, "Ikiwa mnampenda Allah, nifuateni: basi Allah Atawapendeni". Nimechagua baadhi ya nukuu kutoka katika maandishi ya Masih Aliyeahidiwa (a.s). Katika sehemu moja Masih Aliyeahidiwa (a.s) anasema: "Sababu ya mgawanyiko miongoni mwa Waislamu ni mapenzi ya vitu vya kidunia…Masih Aliyeahidiwa (a.s) anasema, "Badala ya Kumpenda Allah Mwenyezi na badala ya kumpenda Mtume Mtukufu (saw), wameyapa kipaumbele mapenzi ya dunia hii. Je huku ndiko kumfuta Mtukufu Mtume (saw)? Je Mtukufu Mtume (saw) alikuwa ni mtu wa kidunia? Je yeye, Allah Aepushie mbali alikuwa na mapenzi ya kidunia au hakuonyesha uzingativu juu ya kutimiza majukuu yake katika Amri za kiroho? Je yeye, Allah Aepushie mbali alikuwa na hata chembe ya unafiki au ulaghai, na je aliitanguliza dunia juu ya dini? Tafakarini juu ya hili! Kumfuta Mtukufu Mtume (saw) maana yake ni kufuata hatua zake na kisha kuangalia ni jinsi gani Allah Mwenyezi atakavyoteremsha baraka zake".

Ingawa, hali halisi ya Waislam leo hii, mfano halisi ulioonyeshwa na Allah Mwenyezi unathibitisha kuwa hali yao ni mbaya zaidi. Nchi zinapigana zenyewe kwa zenyewe. Nchi za Kiislam zinajaribu kuziendea na kuziomba nchi nyingine ziwapige Waislam wa nchi nyingine. Katika siku za hivi karibuni, Rais wa Marekani kwa mara nyingine tena alitangaza

Endelea uk. 11

Ziara za Amir mikoani zaleta neema

- *Kanda ya ziwa yafanya Jalsa na misikiti kufunguliwa*
- *Jamia Ahmadiyya yapata majengo mapya*
- *Shule za Ahmadiyya zaweka misingi ya majengo mapya*

Kwa fadhili zake Allah, mwaka mpya wa jamaat unaoanza kila Julai hadi June umeanza kwa neema. Amir Jamaat afanya ziara katika tarehe za mwanzo za mwaka huu mikoa ya Shinyanga na Simiyu na kuzipatia Jalsa za mikoa hiyo baraka ya uwepo wake. Sanjari na hilo misikiti na nyumba za walimu zilifunguliwa pamoja na wanajamaat husika kufanyiwa matembezi ya kimalezi. Mkoani Morogoro palipatwa na mabadiliko katika chuo cha ubashiri kwa kufunguliwa madarasa.

ZIARA SHINYANGA

Mnamo tarehe 8 Julai wanatawi wa Shinyanga Mjini, Negezi, Shatimba, Ibanza, Mwamidu na wenyeji Bugimbagu walipata kukutana na Amir Jamaat na kufanya nae kikao. Amir Jamaat aliulizia juu ya maendeleo yao katika masuala yote ya msingi ambapo wa akina mama walionekana kuwa mstari wa mbele katika yote yaliyoulizwa. Amir Jamaat aliwahusia wanajamaat kujitahidi kujifunza kwa bidii na kusoma vitabu vya Jamaat ili kuielewa vyema imani yao



Amir Jamaat pamoja na ujumbe wake katika picha ya pamoja na wanajamaat wa Imesela baada ya kufanya kikao nao na kufungua msikiti.

Jamaat ya Songamile ilikuwa mwenyeji wa Jalsa ya Shinyanga iliyofanyika Jumapili 9/7/2017. Mkuu wa mkoa wa Shinyanga Mh Zenab Telak alikuwa mgeni rasmi akiambatana na jopo lililo chini yake la watu takriban 25 lililofanya ionekane kana kwamba serikali yote ya mkoa ilihamia katika viunga vya Jalsa Hotuba ya ufunguzi iliyotolewa na Amir Jamaat ilikuwa na msisitizo " Uislam ni Amani, Hivyo lengo la mkutano wetu huu ni kuhamasisha amani katika jamii kwa kuwakumbusha waumini

Endelea uk. 10